Wakati wa Kanisa La Laodikia

Sasa, kamwe hakumaliza hilo. Nilisema, "Nilichelewa kwenye arusi yangu. . .Nilizaliwa kidogo nimechelewa, nikachelewa arusi yangu kidogo, laiti ningeweza kuchelewa mazishi yangu!" Hayo ndiyo kweli ninayotaka nichelewe, nichelewe kabisa.

2 La, simu zilikuwa zikipigwa nyumbani, nisingeweza kuondoka, ilikuwa vigumu. Kisha baada ya mke wangu na hao wengine kuondoka mapema, nilikuwa tu na mambo mengi sana. Halafu watu mahali mbalimbali, wakiomba, na sasa hivi wakiingia; ndipo ufunuo wa Bwana ukaja kwa ajili ya ndugu fulani; dada amesimama kule nyuma, mgonjwa; mnajua ninalomaanisha, ni kwenda, kwenda, kwenda, kwenda tu. Na hata sijasalimiana na baadhi ya marafiki zangu hapa kutoka Georgia na mahali mbalimbali huku kwote, huko Canada. Ninajisikia vibaya sana kwa kutowapa mkono.

3 Na, jambo lingine, Fred yuko wapi usiku wa leo, Fred Sothmann? Fred, unakumbuka wakati ule uliponipigia simu kutoka Canada, ulipokuwa ukishuka kuja huku, nami nikakwambia usije kwa gari? Ulikuja, hata hivyo; ukapata ajali, karibu . . . aliangamize gari lake, karibu limwue mke wake, familia, akavunja pua yake, na kuwalaza wote hospitalini.

4 Muda mfupi uliopita wakati nilipokuwa nikiondoka, adhuhuri kamili, Ndugu Ben hapa alikuwa amesimama pale nje, akanijia. Kisha Rosella akaja huko, akasema, "Ninaenda nyumbani."

Nikasema, "Rosella!"

Akasema, "Kuna nini, Ndugu Branham?"

Nikasema, "Ninajisikia visivyo kawaida sana juu ya hilo." Mnaona?

Kasema, "Kwani kuna jambo linaloenda kutukia?"

Nikasema, "Sijui. Inaonekana kwangu, kitu Fulani kilinionya."

5 Alinipigia simu dakika chache zilizopita, alipatwa na ajali. Na kwa hiyo, hakuna mtu aliyeumia, bali ilikuwa ni mkono wa Bwana. Naye alikuwa akiteleza (Kumejaa barafu huko Kaskazini.) naye alitelezea Indianapolis, na kuanza kuteleza barabarani upesi sana *hivi*. Ndipo akapaza sauti, "Ee Bwana, nisaidie!" Gari likarudi *hivi* upesi tena, likarudi na kuingia kwenye upande mzuri wa barabara, na kuanza vema. Akapanda

barabarani, akasema, “Jamani, jamani, jinsi ninavyoshukuru kwa kutoka kwenye hiyo, maana magari mengine yanapitia kwenye upande uo huo, yakienda kasi sana.” Kwa hiyo akaingia barabarani, ndipo akasimama huko juu kuninii . . . Ninaamini, kitu fulani, alisimama apate kunywa kikombe cha kahawa ama kitu fulani. Basi kabla hajatoka kwenye gari hilo, gari lingine likagonga papo hapo nyuma yake, lingine papo hapo nyuma yake, lingine moja kwa moja nyuma yake, na yote yakalundikana hapo. Lakini akasema alishtuka kidogo, bali si vibaya, bali alitaka kumshukuru Bwana, na kupiga simu na kuliambia kanisa kumshukuru Bwana kwamba hakuumia wala chochote kile, na akaliomba kanisa liendelee kuomba kwamba atafika nyumbani. Mnaona, yeye ni dereva mpya, ndiyo kwanza apate leseni yake. Kwa hiyo, ninashukuru sana.

6 Lakini daima inafaidi kuchukua maonyo hayo ya Bwana. Kasema, “Vema,” akasema, “Ningepoteza kazi ya siku moja.” Kazi ya siku moja ni nini? Inagharimu zaidi ya hiyo kutengeneza upande wa nyuma wa gari hilo, mnaona. Kwa hiyo ni bora zaidi ku—kukufanya . . . kudumu pamoja na Bwana. Hiyo si ni kweli? Kama akitwambia lolote, afadhali tudumu Nalo. Maana Yeye daima yu sahihi. Sivyo? Sikuzote yu sahihi!

7 Sasa, loo, hii ni ninii sana . . . limekuwa ni juma zuri sana. Kamwe sijui jinsi ya kujieleza kwa Mungu na kwenu ninyi watu kwa ajili ya juma hili zuri sana. Hizi zimekuwa ni baadhi ya siku nane zenye furaha sana kwangu ambazo nimehubri maishani mwangu. Hiyo ni kweli. Nime—nimejifunza sana juu ya Bwana na fadhili Zake, na yote ambayo ametufanyia, na kumwona Roho Wake akitenda kazi kanisani. Nami nina furaha sana kuona karama zikianza kufanya kazi kanisani tena. Mnaona?

8 Sasa, mara zikiwa hapa, wakati umeondoka, inaonekana tu kana kwamba mtu fulani kweli ataingia, ata—ataichafua tu, mwajua, wataanza tu kufanya chochote kile. Basi wakati unapozidharau karama hizo, Mungu atakutahayarisha. Unaona? Hiyo ni kweli. Huna budi kuziweka vizuri. Na, jinsi tunavyotaka ni wakati tu zimewekwa katika utaratibu, jinsi wanavyonena kwa lugha. Sio tu kuyanukuu Maandiko, bali kusema jambo ambalo linakaribia kutukia. Na ikiwa mtaendelea tu kuwa wenye kicho sana kwa jambo hilo, litaanza . . . Kama mtu yeyote akikiuka utaratibu kanisani, Roho Mtakatifu atalizungumzia papo hapo na kuwaambia kwamba yeye ni nani. Na hapo, wata—watajisikia kurudiwa na waende madhabahuni. Hiyo ndiyo kazi ya karama hizo.

9 Na kumwona mchungaji wetu hapa, Ndugu Neville, alikuwa ni mvulana mshamba, mwenye haya. Nami nawaambia, alikuwa . . . ilionekana kana kwamba kamwe hatashikilia ikifikia Pentekoste. Lakini kumwona amesimama na kufasiri lugha na kutabiri, nawaambieni, ametoka mbali. Kweli. Hebu tumwombee mchungaji wetu.

10 Pia, mnaona, karama zinaanza kuja kanisani. Na maskini ndugu mwingine mnyenyekevu hapa, yeye yupo hapa, ana... anapaswa kuwa hapa mahali fulani. Nadhani yupo, yupo sikuzote. Yeye ni maskini jamaa mnyenyekevu sana, alikuwa mmoja wa wadhamini hapa kanisani, Ndugu Higginbotham, mtu wa thamani, mtauwa. Na kuona ya kwamba amepokea karama ya kunena kwa lugha, ni nani angaliweza kuwazia kamwe ya kwamba Ndugu Higginbotham angalifanya hilo? Maskini jamaa mshamba, mwenye soni, hakutaka kujulikana, popote, akikaa nyuma. Lakini, mnaona, Mungu anaweza kumchukua mtu kama huyo na kumtumia, mnaona, maana kwanza kabisa, hataki kufanya hivyo. Kama angalitaka kulifanya, huenda akatokea kuwa ni mtu mwenye kiburi. Lakini mradi tu anafikia ambapo hataki kulifanya, labda Mungu anaweza kumtumia namna hiyo.

11 Junie yupo hapa, yeye ni...loo, yeye yuko nyuma ya hii nguzo kutoka kwangu.

12 Nitasema jambo hili, nimewasikia watu wengi wakinena kwa lugha. Nami nafikiri zote hutoka kwa Mungu, kwa sababu huwezi kutoa sauti pasipo hiyo kumaanisha jambo fulani kwa mtu fulani, mahali fulani. Mwajua, Biblia inasema, "Hakuna sauti isiyo na maana," inamaanisha kwamba hakuna sauti isiyo na maana fulani. Huwezi kutoa tamshi lolote isipokuwa liwe na maana fulani. Daima nilishangaa hilo lingekuwaje mpaka nilipoenda Afrika na kusikia kelele hizo zote, ndipo nikakuta kwamba basi ilikuwa ni sauti ya mtu fulani. Wakati mwingine ni sauti ya kimalaika, na kadhalika.

13 Lakini Junie Jackson, maskini mhubiri wa mashambani wa kanisa la Kimethodisti, mshamba, mwenye soni, mwoga, huko chini—chini kabisa karibu na Elizabeth, Indiana, huko nyuma kabisa mwituni. Mnyamavu, asingesema lolote, kwa namna fulani mshamba, ilionekana kana kwamba...Ningeona wakati mwingine, ninataka kumchukua, nimtikise, niseme, "Sema kitu, Junie, unaona, acha kuketi hapo ukiniangalia tu namna hiyo."

14 Tungeketi juu ya kisiki huko mwituni, naye angeketi pale na kusema, "Vema,...nadhani...ni sawa."

15 Ningesema, "Loo, Junie, na—najisikia kama 'hebu niliseme kwa ajili yako,' unaona. Wewe ni—wewe ni mpole kupita kiasi kwangu, unaona." Naye Mungu akampa ka—ka—karama ya kunena kwa lugha; sijawahi kusikia lugha dhahiri zaidi maishani mwangu mwote. Mnaona?

16 Hebu mwangalieni kanisani. Mlimwona maskini mwanamke yule akinena asubuhi ya leo pasipo kumjua yule mwanamke mwingine? Na pasipo mmoja kumjua mwingine, na huyu, kusikika kwa sauti iliyonenwa kwayo; na wakati yalipofasiriwa, kwa sauti ile ile, irabu, alama za vituo; vile vile hasa, ikirudi. Nao ujumbe huo ulikuwa ni mkamilifu, kwa kanisa. Mnaona jinsi jambo hilo lilivyo? Sasa, inatubidi kumshukuru Mungu.

Sasa, usiweke kifua chako mbele. Ukifanya hivyo, utajiangusha chini, na ibilisi atakushika. Kuwa tu mnyenyekevu; useme, "Ee Bwana, nidumishe nimefichwa, kamwe usiniache niinuke kabla ya wakati."

17 Kamwe hatakuacha ukiuke utaratibu. Kama ukiukiuka, wakati mwingine, hilo halita—hilo halitajalisha. Ukikiuka, mbona, mchungaji hapa ata—atakwambia. Mnaona, ka—karama hazipaswi kuwa wakati mnaninii . . . wakati tukihubiri. Kwa kawaida, kama karama zikianza kufanya kazi vizuri kanisani, tutawahimiza mkutane muda mrefu kabla ya ibada hiyo nyingine; mumruhusu Bwana afanye kazi nanyi pale, mnaona, maana basi kwenye sehemu hii haitakatiza hata kidogo. Sasa, wakati tukiwa kwenye kusanyiko, wakati mwingine inakubidi kutulia kidogo. Lakini ikiwa Mungu ana ujumbe, mahali fulani ama pengine Yeye atautoa, mnaona, achana tu na Yeye, bali lifanye kulingana na mafundisho ya Biblia. Basi Ndugu Neville labda atakuwa akifundisha juu ya mambo hayo, ambayo tutajaribu kufanya. Nitajaribu kuendelea kumsaidia tuwezavyo, sote wawili pamoja, kulifafanua na kuwaonyesha jinsi inavyopaswa kutumiwa.

18 Je, unajisikia afadhali zaidi, ndugu yangu Mpolandi? Hiyo ni sawa. Loo, jinsi Bwana alivyombariki! Miaka minane iliyopita, nilimwambia jambo fulani lingetukia. Alikuwa amechanganyikiwa kabisa, mwana utatu shupavu. Naye Bwana alisema, hivi majuzi, "Kuna mtu ajaye, ana nywele nyeusi na macho ya hudhurungi, mnene. Usimfukuze, ninamtuma kwako." Nikachukua Andiko mahali pale hasa alipokuwa amechanganyikiwa, nikaandika kijipande cha karatasi na kukiweka pale. Baada ya kitambo kidogo huyu hapa anakuja.

Mke wangu akasema, "Yupo mtu huko nje kukuona."

Nikasema, "Huyo ndiye, mkaribishe ndani."

19 Ndipo a—akaniambia aliyoambiwa katika . . . chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu. Jinsi ambavyo sikuzote aliamini na kuushikilia Ujumbe, na kadhalika, miongoni mwa watu wake; ingawa alikosolewa, alidumu Nao kabisa. Kasema, siku moja, mkutanoni, kwamba nilimzungumzia na kuliita jina lake. Na jinsi nilipata kutaja jina hilo, sijui mimi. Alisema ilinibidi ku—kuliendelezea herufi, ama kitu kama hicho, mkutanoni. Kasema alikuwa amembeba mtoto mkononi mwake aliyekuwa na vidonda usoni mwake, naye akasema mtoto huyo mchanga alitakaswa kabisa, kikamilifu tu. Na jinsi ambavyo Bwana . . .

20 Basi nikasema, "Vema, kile unachohitaji sasa ni kushuka uende kanisani ukabatizwe katika Jina la Yesu Kristo."

21 Nilikutana naye muda mfupi uliopita juu ya mlima, maana alishuka, akabatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Sasa ameridhika kabisa, anajisikia vizuri, anarudi nyumbani. Natumaini atanifasiria huko Uholanzi moja ya siku hizi, na

Ujerumani, na katika, huko nyuma katika sehemu hizo. Bwana akubariki, ndugu yangu.

22 Mambo mengi sana mazuri ambayo Bwana hufanya! Kuona tu rehema Zake—Zake, jinsi ambavyo kutoka mashariki, magharibi, kaskazini, na kusini, Yeye anawaongoza watoto Wake wapendwa; wakiunganika, wakitoka, wakijitikisa kabisa. Mengi sana ya kusemwa!

23 Sasa, msisahau, Jumapili ijayo usiku, Bwana wetu akipenda, Jumapili ijayo usiku, tutakuwa na. . . Jumapili ijayo asubuhi, hasa, ibada ya uponyaji. Sababu ya mimi kusema hilo juu ya hilo, labda basi ikiwa kutakuwako na wengi kupita kiasi Jumapili asubuhi nitachukua Jumapili usiku kuendelea nayo, mnaona. Bali kama ninaweza kuwapata wote Jumapili asubuhi, vema, sawa.

24 Jumatano usiku ni mkutano wa maombi wa katikati ya juma. Sasa, kwenu watu mlio hapa karibu na nyumbani, ninyi jamaa mnaokutanika hapa, fanyeni mkutano wa maombi. Msiukose huo, dumuni moja kwa moja nao, mnaona. Na muombe, mtafute kumkaribia Mungu. Kamwe msiache ushupavu uingie miongoni mwenu. Ninii. . . Kuna mengi mno kupita kiasi yaliyo halisi kukubali ya uongo, mnaona, msi—msiingie upande mbaya. Dumuni wakweli.

25 Nilisikia "Amina" inayojulikana basi ambayo nimeisikia kwa miaka kadha wa kadha, Ndugu Russell Creech. Wananiambia ya kwamba Patty ndiye aliyekuwa akinena kwa lugha kule nyuma hivi majuzi usiku. Patty, uko wapi? Uko hapa, kipenzi? Naam, jamani, hata nisingemjua kama ningemwona. Lakini ninaamini nilimshika mtoto huyo kwa mikono yangu na kumweka wakfu kwa Bwana, papa hapa. "Naye ni mwanamke kijana," Meda alisema, "maskini msichana tineja, mrembo," nguvu za Roho Mtakatifu zikiwa juu yake, akinena kwa. . . Russell, wewe ni tajiri. Naam, wewe ni tajiri.

26 Yuko wapi Dada Creech? Sijamwona. Yuko? Huko nyuma. Loo, Dada Creech, jinsi ninavyoshukuru kwamba Mungu amekupa mtoto kama huyo, mbona, hutambui jinsi—jinsi ninavyoshukuru. Kwenye wakati ambapo wasichana matineja wanacheka kichinichini na kucheka na kuendelea, unajua, pamoja na lundo la upuuzi kwa jamaa hawa, mtindo wao wa kukata nywele kama bata na kila kitu, na jinsi hiyo; naye maskini mtoto huyu hapa mwenye nguvu za Roho Mtakatifu, akinena kwa lugha hapa. Loo, jamani!

27 Hmm! Ni wanaume wangapi usiku wa leo, wahubiri wa Kipentekoste, ambao wangeyatoa maisha yao yote kama wangeweza kuona binti yao tineja, ambaye yuko huko nje kwenye karamu ya roki, akifanya hivyo.

28 Hebu ta—tathmini tu hilo, ndugu. Ninajua yale unayofanya kule kwenye Barabara Kuu, nilifanya jambo lile lile, nilifanya

kazi siku nyingi ngumu, lakini, ndugu . . . kuwalea hao watoto. Lakini kumbuka, Mungu ni mwaminifu, Yeye hujazi. Naam, kweli! "Nitalipa."

29 Mungu akubariki, Patty. Kipenzi, ni—nisingekujua kama ningalikuona, nadhani, bali kamwe usiiache njia hiyo nyofu, kipenzi. Kamwe usiache ibilisi aweke chochote—chochote ndani yako, kama tofaa zuri la dhahabu, kwa sababu litakuwa ni limau, unaona. Kiangushe kitu hicho na ukiache namna hiyo. Elekeza macho yako moja kwa moja kwa Kristo, moja kwa moja Msalabani. Na uendelee kusonga mbele, kwa kuwa saa imekaribia. Unaona?

30 Mambo mengi sana ya kusihi ningeweza tu kusema, baraka za Mungu. Sikuwa nimeweza kuwatembelea wengi, na juma hili lote sijaombea zaidi ya watu hamsini, nadhani, na kuingia na kutoka, na mambo ya dharura na yale yanayokuja, na kadhalika, bali nimekuwa nikisoma. Lakini sasa, Jumapili ijayo, tutakuwa tukiwaombea watu, na kumwomba Bwana ashuke na kutupa nguvu kuu, na kujidhihirisha Mwenyewe kwetu Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda.

31 Loo, ninachukia tu kuanza kwenye wakati huu wa kanisa kwa sababu ninajua ndio wa mwisho wa hizo. Na sasa, katika huu, utakuwa ni ku—kumalizia kwa zile Nyakati Saba za Kanisa. Mmezifurahia? [Kusanyiko linaitikia, "Amina!"—Mh.] Sasa, kumbukeni, ninasema hili mwishoni kama nilivyosema mwanzoni, huenda kukawa na mambo mengi—huenda kukawa na mambo mengi ambayo hamkubaliani nami kabisa, bali msiyashikilie dhidi yangu, mnaona. Nipendeni tu, kwa vyovyote vile, kwa sababu haitaleta tofauti yoyote yale mtakayofanya au mtakayosema, nitawaza vivyo hivyo tu juu yenu; kwa vyovyote vile, zaidi, mnaona, kwa vyovyote, ningewapenda zaidi. Bali nawapenda, Mungu anajua hilo, hakuna mtu ambaye angeliitia Jina la Yesu Kristo ila yule ambaye ningempenda. Mnaona?

32 Wala kamwe sitaki chuki yoyote wala kutojali, ingawa tungekosana kabisa. Kama tulikuwa tumeketi mezani na mmoja anakula aina moja ya sambusa, na mmoja, nyingine, hiyo ingekuwa ni kama papa hapa, mnaona. Inapofikia ushirika mmoja na mwingine, tunapendana. Na tusipopendana, basi tunapaswa kupendana. Na endapo . . . kamwe hatutapiga hatua katika Mungu mpaka tutakapofanya hivyo.

33 Kamwe msisahau, msisahau ya kwamba karama iliyo kuu kuliko karama zote ni upendo. "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na malaika, niutoe mwili wangu ukachomwe moto kama sadaka, nijapofahamu maarifa yote, na kadhalika, si kitu mimi. Kwa hiyo . . . Lakini wakati kile kilicho kikamilifu, ambacho ni upendo . . . " Kama karama zote za kiroho hazijatiwa saruji kwa upendo, hazitadumu. Saruji nyingine yoyote

itapasuka, "Bali upendo huendelea milele." Mnaona, hiyo ni Wakorintho wa Kwanza 13.

34 Sasa, usiku wa leo, tunapoingia kwenye wakati huu mkuu wa kanisa. Loo, jamani! Sasa, huenda tukawa kwenye saa tatu (usiku wa leo) na robo. Na sasa hakika ninasikitika kwamba hatuna nafasi ya kutosha, bali . . . kuketisha kila mtu, kuwaketisha watu wote, hasa, bali kweli hatuna, na labda siku moja tutakuwa nayo.

35 Lakini sasa ninataka kuwaomba mnifanyie fadhili. Mnaona msimamo wangu na mnajua utakachonigharimu siku moja, mnaona, na wakati huo umekaribia. Mnaona? Sasa, ninawatakeni mfanye hivi, sikuzote niombeeni. Pia kumbukeni, nimekuwa mwaminifu jinsi nijuavyo kuwa mwaminifu, mnaona. Nami ninatambua mimi si mtoto tena, nina umri wa miaka hamsini na mmoja. Na mimi—mimi wakati ninii yangu . . . Siwezi kuondoka mpaka Mungu atakaponiita. Nami nitaenda jinsi anavyonitaka niende, na itakuwa hivyo. Mnaona? Lakini sina budi kuwa mwaminifu na kusema Kweli, haidhuru. Kwa hiyo ninajua wakati mwingine ni njia ya upweke, lakini mradi Yeye yuko pamoja nawe, inaleta tofauti gani? Mnaona?

36 Sasa, kabla hatujaingia kwenye wakati huu mkuu wa kanisa, sijui kama tungesimama kwa ajili ya maombi, kwa muda mfupi tu tena. Hiyo kwa namna fulani inakuruhusu kujinyosha na kujisikia vizuri zaidi. Kwenye ibada ya kumalizia, je, kuna . . . Ni wangapi hapa wangetaka kukumbukwa mbele za Mungu? Mwinulieni tu Mungu mikono yenu, "Unikumbuke, Ee Bwana, mwishoni mwa wakati. Wakati maisha yamekwisha kabisa, unikumbuke."

37 Baba yetu wa Mbinguni, hatuna ndimi za kutosha kuelezea shukrani zetu kwa ajili ya Uwepo wa Mungu aliye hai ambaye amekuwa miongoni mwetu juma hili lililopita, kwa ajili ya mambo tuliyojifunza Kwako, jinsi ambavyo umejifunua Mwenyewe kwetu kote katika wakati, na jinsi ambavyo umelifanya Neno Lako dhahiri sana kwetu. Jinsi ambavyo tumekungojea Wewe, na jinsi ambavyo tume—tumejaribu kuonyesha upendo wetu, na kushindwa kufanya hivyo, Bwana, maana ndimi za wanadamu zisingeweza kufanya hivyo. Ku- . . . hata kwa ajili ya kutuokoa, na Wewe . . . hata kwa kutupa njaa kwa ajili Yako. Kwa kuwa imeandikwa katika Neno, "Heri wenye njaa," (kuona njaa tu, ni baraka) "njaa na kiu ya haki." Halafu ukatoa lile tamshi kuu, "Kwa kuwa watajazwa!" Sasa, tunaamini hilo, Bwana. Tusamehe kupungukiwa kwetu.

38 Na tunapoingia usiku wa leo kwenye . . . kwenye wakati huu wa mwisho wa kanisa, ambao ni Laodikia, baada ya kuyaona Maandiko na historia zikiafikiana kikamilifu kila wakati. Kwa hiyo, Baba, tunajua nukuu hili kutoka kwenye unabii Wako mkuu hapa, wa wakati huu wa mwisho, utakuwa tu

kama nyakati zile zingine sita zilivyokuwa. Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utamwacha Roho Mtakatifu aje kwetu usiku wa leo, sasa, na kutubariki wakati tukiendelea kukungojea Wewe. Katika Jina la Yesu. Amina. Ketini.

39 Bwana akipenda, kitabu kitaninii. . .punde tuwezavyo. Ndugu Leo anayatoa kwenye kanda ya sumaku, yaingie kwenye. . .yaingie kwenye hati ya mkato, kutoka hapo yakapigwe chapa, kisha kuingia kwenye kitabu.

40 Na jambo lingine, Rosella atatoa kitabu chake karibuni sana, *Mlevi Sugu Kaokoka*. Ninyi nyote mnaikumbuka hadithi yake, jinsi ambavyo Roho Mtakatifu alimwita mkutanoni. Naye alikuwa. . .alikuwa amekatiwa tamaa na mashirika manne yaliyo makubwa mno ya walevi sugu, kisha akafukuzwa kwenye hospitali zilizokuwako huko Chicago. Naye Bwana Yesu, kwa muda wa dakika moja, alimwondolea yote. Yeye huenda tu kutoka gereza hadi mahali pengine, akiwaambia watu jinsi Mungu awezavyo kukomboa, akizungumza na walevi sugu na kadhalika. Amekuwa. . .kwa ushuhuda wake, amewaleta watu wengi kwa Kristo.

41 Sasa, wakati wa kwanza wa kanisa, je, mwaweza kuniambia ulikuwa ni upi? Efeso. Wa pili? Smirna. Wa tatu? Pergamo. Wa nne? Thiatira. Wa tano? Sardi. Wa sita? Filadelfia. Wa saba? Laodikia.

42 Wa kwanza ulikuwa kati ya A.D. 55 na 170, Efeso. Smirna, 170 hadi 312. Pergamo, 312 hadi 606. Thiatira 606 hadi '520. Sardi, '520 hadi 1750. Filadelfia, 1750 hadi sita. . .'06; sasa, ulianza wakati wa Laodikia, ukaingiana, na jana usiku tuliingia kwenye huku kuingiana kidogo. Sasa, usiku wa leo, tutachukua mwisho wa Laodikia.

43 Tunaamini ya kwamba kanisa la Laodikia lilianza A.D. 1906. Ninabashiri. . .Sasa, kumbukeni, "kubashiri," hasa sana ninyi mnaosikiliza kwenye kanda. Sisemi itakuwa hivyo, bali ninabashiri ya kwamba utaisha kufikia 1977, ya kwamba kanisa litaingia kabisa katika ukengeufu nalo litatapikwa kutoka kinywani mwa Mungu. Na kule Kuja kwa Pili, ama Kunyakuliwa kwa Kristo, kunaweza kukaja wakati wowote. Sasa, ningeweza kukosa hilo kwa mwaka mmoja, ninaweza kulikosa kwa miaka ishirini, ningeweza kulikosa kwa miaka mia moja. Sijui mahali hilo. . .Bali ninabashiri tu ya kwamba kulingana na ono alilonionyesha, na nikiuchukua huo wakati, jinsi mambo yanavyoendelea, ninasema itakuwa wakati fulani kati ya '33 na '77. A—angalau, taifa hili kuu litaingia kwenye vita vitakavyolilipua vipande-vipande, mnaona. Sasa hiyo ni karibu sana, imekaribia sana. Nami ningeweza kukosea, ninabashiri. Je, kila mtu anaelewa? Semeni "Amina" ikiwa mnaelewa. [Kusanyiko linasema "Amina!"—Mh.] Mnaona?

44 Lakini Bwana alinionyesha ono la mwanamke mkuu mwenye nguvu, katika mwaka wa ’33, 1933, liko kwenye gazeti. Jinsi ambavyo “Roosevelt angesababisha . . . angesaidia kuingiza ulimwengu vitani.” Jinsi ambavyo “Mussolini angefanya uvamizi wake wa kwanza Ethiopia naye angeiteka, bali angefikia mwisho wenye aibu.” Na jinsi ambavyo “Halafu zile itikadi tatu: Unazi, Ufashisti, na Ukomunisti, zote zingeishia kwenye Ukomunisti.” Basi ni wangapi hapa ndani wanaonikumbuka nikininii tu . . . nikiwafanya msimame, na kulirudia-rudia, ningewaambia, “Itazameni Urusi! Itazameni Urusi, mfalme wa Kaskazini! Itazameni Urusi, mfalme wa Kaskazini! Itazameni Urusi, mfalme wa Kaskazini!”? Ni wangapi wamenisikia nikisema tu, peperusha hicho, tena? Watu wa zamani, mnaona, huku nyuma sehemu ya mwanzoni mwa kanisa hili. Kusimama tu pale na kulipeperusha tena na tena, “Itazameni Urusi, mfalme wa Kaskazini! Mnaona, kile angefanya, kwa kuwa itikadi hizo zote zitalundikana katika Urusi.”

45 Kisha nikasema, kwamba “Taifa hili hatimaye lingeingia katika vita na Ujerumani. Nayo Ujerumani ingejenga ukuta wa saruji.” Na huo ulikuwa ni ile Ngome ya Maginoti, miaka kumi na mmoja kabla haijaanza kujengwa, miaka kumi na mmoja kabla. Kisha nikasema, “Wamarekani watapigwa sana huko kwenye ngome hiyo.” Baadhi ya hawa ndugu hapa walikuwa kwenye hiyo ngome, Ndugu Roy Roberson na hao wengine; hebu waulizeni kilichotukia. Hakika walipigwa. Vema. “Lakini hatimaye,” nikasema, “tutashinda na tutakuwa mmoja wa washindi katika vita kati yetu na Ujerumani.”

46 Sasa, nilisema, “Ndipo baada ya wakati huo, ya kwamba sayansi itapiga hatua kwelikweli.” Walipiga, waliunda bomu la atomiki na kila kitu. Nikasema, “Wakati wa mafanikio yao, wangetengeneza . . . magari yangeendelea kuchukua umbo la yai.” Nanyi mnakumbuka maskini ile boneti kubwa ya kale kwenye 1933, upande mkubwa wa nyuma ulishuka namna hii, gurudumu la spea nyuma yake? Angalieni jinsi lilivyo sasa, mnaona: limenyoshwa, mnaona, kama yai. Kisha nikasema, “Hatimaye watavumbua gari ambalo haitawabidi kuwa na usukani ndani yake. Niliona familia moja ikiteremka kwenye . . . Naiita, ‘barabara,’ katika gari lenye kioo upande wa juu, barabara kubwa mno zilizoonekana nzuri na gari zuri. Nao walikuwa wameketi, wakitazamana, nalo hilo gari lilikuwa likijiendesha lenyewe, likipiga kona moja kwa moja na kila kitu.” Nao wanalo hilo gari sasa hivi, tayari limevumbuliwa. Wanalo hilo gari. Ndipo nikasema basi, “Loo, jinsi ambavyo sayansi itaendelea katika siku hiyo!”

47 Nikasema, “Kisha nikaona . . . Watawaruhusu wanawake na wanawaruhusu wanawake kupiga kura. Na kwa kupiga kura, watamchagua mtu asiyefaa moja ya siku hizi.” Nanyi mlifanya

hivyo katika uchaguzi huu wa mwisho. Kura za wanawake ndizo zilizomchagua Kennedy. Tunajua hilo, mnaona, kati ya mitambo mibovu na vitu vilivyopangwa kijanja, ambavyo FBI lilifichua. Basi mtu yeyote angewezaje...Mbona hawafanyi lolote kulihusu? Kwa nini halisemwi lolote? Haa! Wanahofu mtu fulani atapoteza kazi yake. Mnaona, ni lundo tu la siasa, imeoza kabisa. Hivyo tu. Hakika!

48 Hakuna—hakuna...hakuna, samahani. Hakuna wokovu katika taifa hili, hakuna wokovu katika taifa lolote. Wokovu uko katika Yesu Kristo na Yeye pekee! Uh-huh! Hiyo ni kweli. Sasa, ninashukuru kwa ajili ya Marekani. Afadhali niishi hapa kuliko mahali popote ulimwenguni, kwa sababu...nje ya Canada. Canada na Marekani ni mapacha, tunajua hilo, mataifa jirani, mahali pazuri sana, bali ni—ninaamini afadhali niishi hapa kuliko mahali pengine popote nipajuapo, kwa sababu ni nyumbani kwangu. Nina furaha kwamba mimi ni Mmarekani, na ninashukuru kwa ajili yake. Bali nawaambia, hakika inahitaji uamsho mwingine, hakika inahitaji. Ila haitaupata! La, bwana. Kamwe halitasimama tena! La bwana. Limekwisha! Mnakumbuka, yapata miaka mitano iliyopita huko Chicago, hilo liko kwenye kanda. Unayo, Gene. Nilisema, "Ama wataikubali mwaka huu, au wataendelea kushuka chini." Nao wamefanya hivyo, mnaona, nao watafanya hivyo mpaka hatimaye itakutana na mwisho wake.

49 Lakini kutakuwako na mwanamke mwenye nguvu! Sasa, kumbukeni! Hili liko kwenye kanda, pia. Mwanamke mwenye nguvu, mwanamke mashuhuri, ama atakuwa ni Rais, au itakuwa ni mwanamke anayewakilisha kanisa Katoliki (ambalo nafikiri ndilo) atachukua mamlaka hapa siku moja naye ataitawala nchi hii. Taifa hili ni taifa la mwanamke. Bendera ilitengenezwa na mwanamke, ni namba kumi na tatu. Lilianza, nyota kumi na tatu, milia kumi na mitatu, koloni kumi na tatu. Kila kitu ni kumi na tatu, kumi na tatu, kumi na tatu, moja kwa moja hivyo. Nyota kumi na tatu kwenye dola yake ya fedha sasa. Kila kitu ni kumi na tatu. Ni namba kumi na tatu, na linaonekana katika mlango wa 13 wa Ufunuo. Kumi na tatu kabisa! Kila kitu ni "mwanamke, mwanamke, mwanamke, mwanamke, mwanamke," moja kwa moja kuendelea. Naye alichukua ofisi zote. Amechukua Hollywood. Ameyachukua mataifa. Amezichukua ofisi. Amechukua kila kitu kilichopo; haki sawa na mwanamume, anapiga kura pamoja na wanaume, hulaani kama mwanamume, hunywa pombe kama mwanamume, chochote kingine. Na ni chambo tu kwa kanisa Katoliki, kwa ajili ya kuabudiwa kwa mwanamke! Tayari wanamwabudu mwanamke, kwa vyovyote vile.

50 Yeye ndiye aliye bora sana...Mwanamke mzinifu ndicho chambo kizuri kuliko vyote ibilisi alichopata kuwa nacho. Yeye

ni mbaya kuliko baa zote zilizowahi kuwapo. Anaweza kupeleka watu wengi kuzimuni kuliko baa zote nchini. Hiyo ni kweli.

51 “Mwanamke mwema ni kito kwenye taji ya mwanamume,” kasema mtu mwenye hekima kuliko wote duniani. Mwanamume anapaswa kumheshimu mwanamke mzuri, mnaona. “Bali aliye mwovu ni maji damuni mwake,” nayo damu yake ndiyo uhai wake. Ninyi wanaume mlio na wake wazuri, hamjui jinsi mnavopaswa kumshukuru Mungu kwa ajili ya mke mwema! Kwa kuwa kama Mungu angaliweza kumpa mwanamume chochote kilicho kizuri zaidi kama msaidizi, angalimpa. Lakini mwanamke ndiye msaidizi mzuri kuliko wote ambaye Mungu angeweza kumpa mwanamume. Lakini wanapogeuka . . .

52 Yeye ndiye ambaye katika bustani ya Edeni Shetani alimchagua kama chombo chake. Hakumchukua mwanamume, alimchukua mwanamke. Kwa nini hakwenda kwa Adamu akampe hisia? Alikuja kwa mwanamke na kumpa, mnaona, maana huyo ndiye aliyemchagua. Mungu alimchukua mwanamume, na Shetani akamchukua mwanamke.

53 Basi angalieni moja kwa moja hata chini, na mwishoni . . . Wakati Babeli ilipoanzishwa hapo mwanzo, *Babeli Mbili* kilichoandikwa na Hislop, mwanamke! Inapofikia kwenye wakati huu; sasa inaumalizia wakati wa Mataifa. Babeli ilianza namna hiyo, nayo inaishia kwa ibada ya mwanamke (Mariamu) kanisani. Ni siku ya jinsi gani tunayoishi!

54 Sasa, *Laodikia*, wa—wakati wa Laodikia, hilo neno linamaanisha “vuguvugu.” Umejitajirisha, nao unafikiri hauna haja ya kitu. Bali Biblia inasema ya kwamba ni “mnyonge, kipofu, mwenye mashaka, na uchi.” Ni hali ya jinsi gani!

55 Zawadi kwa wale wanaoshinda katika wakati huu wa kanisa, ni “kuketi kwenye kiti cha enzi pamoja na Bwana.”

56 Sasa, nyota, ama malaika, ama mjumbe wa wakati huu wa kanisa, hajulikani.

57 Sasa, mjumbe wa wakati wa kwanza wa kanisa, huyo alikuwa ni nani? Paulo, Efeso. Smirna? Ireneo. Pargamo? Mtakatifu Martin. Thiatira? Columba. Sardi? Luther. Filadelfia? Wesley. Na katika . . . Laodikia hii, hatujui bado, na labda hatutajua mpaka utakapokwisha.

58 Ila ningetaka tu kutoa nukuu yangu ya jinsi malaika huyu atakavyokuwa, kile tunachotarajia. Hilo lingekuwa ni sawa? [Kusanyiko linasema, “Naam! Amina!”—Mh.] Kwa kuwa tuna muda mfupi, niliandika tu nukuu ndogo hapa yale niliyowazia.

59 Malaika wa kanisa hili la Laodikia, kulimalizia. Sasa, atakuwa kwenye mwisho wa wakati, kama hao wengine, kama vile Biblia. Atakuwa kwenye mwisho wa wakati. Si mwanzoni mwake, mwishoni mwake, kwa sababu malaika daima huja kukemea kwa ajili ya . . . kuwakemea kwa yale

waliyofanya. "Kwa—kwa malaika wa kanisa la Laodikia andika mambo haya."

60 Mnaona, "Kwa malaika wa kanisa la Smirna andika mambo haya." Mnaona, kila moja ni kwa malaika mwishoni mwa wakati. Paulo, mwishoni mwa wakati. Na kuendelea, mwishoni mwa wakati. Kule kuingiana, mwishoni mwa wakati. Mwishoni mwa wakati, hilo ndilo linalozifanya ziingiane. Mnaona, "Kwa malaika," akinena yaliyokuwamo. Huu unaingiana hapa, "Kwa malaika," mwishoni mwa wakati huo. Mnaona, ukichukulia papa hapa, uliingiana kama vipandio vinavyopanda juu, zile Nyakati Saba za Kanisa.

61 Sasa, malaika huyu anayekuja katika siku hii, ninataka . . . Nina kitu kilichoandikwa hapa, ningependa kukisoma tu. Bali atajulikana kwenye sehemu ya mwisho ya wakati. Na kwa sababu tuko karibu sana na huo—karibu sana na huo wakati wa Nuru, hata labda yeye yuko duniani sasa. Unaona, hatumjui. Atakuwa na—nabii mwenye nguvu ambaye atakataliwa na kanisa la ulimwengu, kwa kuwa wataendelea moja kwa moja katika dhambi zao na hatimaye watapikwe kutoka kinywani mwa Mungu, kutoka kinywani mwa Uwepo wa Mungu.

62 Ninaamini atakuwa mtu kama Eliya. Nitatoa sababu zangu ni kwa nini. Sasa, hebu tufungue tu hapa katika Kitabu cha Malaki, kwa muda mfupi tu, nitawapa ni kwa nini nafikiri itakuwa ni mtu aliyepakwa mafuta kwa Roho ya Eliya. Sasa, nawatakeni mvae kofia yenu—yenu ya neema sasa. Malaki, mlango wa 4. Sasa, sikilizeni ninaposoma, nanyi katika Biblia yenu. Sasa, wazieni kwa makini sana sasa kwa dakika chache zifuatazo, sasa, kabla hatujaingia kwenye wakati wa kanisa.

> *Kwa maana, angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, naam, . . . wote watendao uovu, watakuwa* makapi: *na siku ile inoyokuja itawateketeza, asema* B*WANA* *wa majeshi,* na *haitawaacha shina wala tawi.*

63 Yeye anasema nini? Ananena juu ya siku inayokuja. Mtakubaliana na hilo? Siku ya kuja kwa Bwana.

> *Lakini kwenu . . .*

64 Sasa angalieni, sasa Yeye anazungumzia Israeli. Sasa, Yeye alisema nini? "Kwa maana, angalieni, siku inakuja (huko mbali) itakayowaka."

> *Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langu . . . Jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake; nanyi mtatoka nje, na kucheza-cheza kama ndama wa zizini.*
>
> *Nanyi mtawakanyaga waovu; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu katika siku i- . . . siku ile nifanyayo, asema* B*WANA* *wa majeshi.* (Sio . . . Ile

siku ambayo Yeye ataiteketeza dunia, tutayakanyaga majivu yao. Hiyo ni ule Utawala wa Miaka Elfu, bila shaka, mnaona.)

Ikumbukeni. . .*torati ya Musa, mtumishi wangu, niliyomwamuru*. . .*huko Horebu kwa ajili ya* Israeli *wote, naam, amri na* hukumu.

Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja. . .na *siku ya Bwana, iliyo kuu na kuogofya.*

Naye ataigeuza mioyo *ya baba iwaelekee watoto wao, na* mioyo *ya watoto iwaelekee baba zao; ili nisije nikaipiga dunia kwa laana.*

Mwisho wa Agano la Kale.

65 Sasa, Yesu alisema. . .Mathayo 17:10, akinena juu ya hili. Wayahudi wote wanamtazamia huyo Eliya ajaye. Sasa, angalieni yale Yesu aliyosema kuhusu hilo, Mathayo 17:10. Tutaanzia kwenye kifungu cha 9, Mathayo 17:9:

Na walipokuwa wakishuka mlimani, Yesu aliwaagiza, akasema, Msimwambie hata mtu. . .*Msimwambie mtu yeyote habari ya maono hayo,* (Mnaona, "Msiseme haya. Mnayajua, bali msiyatangaze.") . . .*Msimwambie* mtu ono hili, *hata Mwana wa Adamu atakapofufuka*. . . *katika wafu.* Msilitangaze.

Wanafunzi wake wakamwuliza, wakisema, Basi kwa nini waandishi hunena *ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza?* Kwa nini Eliya hana budi kuja kabla ya huyu Kristo kuja, Jua la haki? Kwa nini wakasema hivi? Hapa, Wewe tayari upo hapa, nao waandishi walisema kwamba—kwamba imempasa Eliya kuja kwanza.

Sasa, angalieni:

Naye akajibu akawaambia, Kweli Eliya yuaja, *yuaja kwanza, naye atatengeneza yote.*

Ila nawaambia, Ya kwamba Eliya amekwisha kuja, wala hamkumtambua, (Mnaona, Yeye hakusema kwamba alikuwa ni nani, mnaona.) *lakini wakamtenda yote waliyotaka. Vivyo hivyo Mwana wa Adamu naye yuaenda kuteswa kwao.*

Ndipo wale wanafunzi walipofahamu ya kuwa amesema nao habari za Yohana Mbatizaji. (Sasa—sasa, Yohana Mbatizaji alikuwa ndiye Eliya aliyekuwa aje.)

66 Sasa angalieni, ninarudi kwenye Malaki mlango wa 4, tena. Sasa kumbukeni, Yeye alisema hapa ya kwamba "Kabla haijaja ile Siku ya Bwana, iliyo kuu na nzuri, ya kuogofya, nitawapelekea Eliya nabii." Kifungu cha 5:

> Bali *nitawapelekea* ninyi . . . *nabii* . . . *nitawapelekea Eliya nabii kabla haijaja siku ile iliyo kuu na ya kuogofya ya* . . . [Kusanyiko linasema, "*Bwana!*"—Mh.]

67 Tunaona nini "katika Siku ya Bwana"? Mwishoni mwa wakati! Hapo ndipo ulimwengu utakapochomwa moto. Mnakumbuka jinsi tulivyomchukua akiwa amevaa wigi nyeupe, mwajua, na—na kifua Chake, huku amefungwa kwenye kifua. Mnakumbuka hilo? Nasi tulithibitisha kwa Biblia, haikuwa siku ya *sabato* wala *Jumapili*, ilikuwa ni Siku ya Bwana. Hiyo ni kweli? Na hiyo ndiyo siku anayokuja kama Hakimu, "Naye ataipiga dunia kwa laana." Hiyo ni kweli?

> Nami *nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na kuogofya:*

68 Sasa, angalieni kule kuja mara mbili kwa Eliya. Sasa, kama utaangalia, Maandiko yote yana maana maradufu, "Ila yamefichwa macho ya wenye akili na maarifa, yakafunuliwa watoto wachanga watakaojifunza." Hivi hamuamini hilo? Sasa, shikilieni Malaki 4 papo hapo.

69 Na sasa hebu turudi kwenye Mathayo 2 kwa dakika moja tu, papo hapo tu upande wa pili wa ukurasa, Mathayo 2. Ninaamini ilinipasa kumaanisha Luka 2 badala ya Mathayo 2. Nimeiandika hapa chini, bali nilikuwa nikiharakisha dakika chache tu zilizopita, naye Roho Mtakatifu alikuwa chumbani juu yangu nami nilikuwa na wakati mzuri sana. Kwa hiyo nilimaanisha . . . 2, hebu tuone kama hapa pangekuwa ndipo. Sasa, hebu nisome hapa kwa dakika moja. Mathayo 2? Hapo sipo ninapoangalia, sivyo? Sasa, hebu kidogo, nitapapata katika ninii tu . . . Hebu nipate wakati kidogo tu hapa maana ninawatakeni mwe na hakika kuliona, kwamba Maandiko yana maana maradufu Kwake. *Kusujudu kwa Hana; Kurudi Nazareti; Pasaka; Huduma ya Yohana*. Sasa, hebu nione kama ningalimaanisha Luka, nilikuwa nikisoma mahali fulani na . . . Ni—ninamaanisha Marko badala ya Luka, huenda ilikuwa ni Marko. Lakini ninawatakeni mlipate Andiko hili ili kwamba— ili kwamba mweze kujua kwamba ni kazi ya Bwana, ya kwamba Yeye kweli hufanya jambo hili kwa njia hii. Sasa, nitawaambia mahali ninapopatafuta, ambapo ninii, "Kutoka Misri nimemwita mwana Wangu." Kuna mtu aliye na maandiko ya pambizoni ambaye anaweza kulipata upesi sana ama kuliona? "Kutoka Misri nimemwita Mwanangu, nimemwita Mwanangu." Sasa, hebu kidogo.

70 [Ndugu fulani anasema, "Luka 1:17."—Mh.] Luka 1:17. Asante, ndugu. Hiyo ni kweli, Luka 1. Marko . . . Luka 1:17, badala ya 2. Ninataka kufungua cha 14, hapo ndipo . . . Hicho ndicho, ndugu. Hicho ndicho kabisa, Luka 1:17. Vema. Sasa, unaweza kukiandika. Sasa, jambo ni kwamba, ni kutoka kwa baraka za Bwana, ambapo lilibarikiwa.

Nawe utakuwa na furaha na shangwe; na watu wengi watakufurahia kuzaliwa kwake.

Kwa sababu atakuwa mkuu mbele za Bwana, hatakunywa divai wala kileo;

71 Mtu huyu anayekuja atafundishwa tangu kuzaliwa kwake asinywe wala kuwa na uhusiano wowote na dhambi kama hiyo. Mnalipata?

. . . naye atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye.

Na wengi katika Waisraeli atawarejeza kwa Bwana Mungu wao.

Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya, na nguvu zake, ili kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na kuwatilia waasi akili za wenye haki; na *kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa.*

72 Sasa, sasa tunatambua ya kwamba alitabiriwa, naye Yohana alikuwa ndiye mtu huyo! Hiyo ni kweli? Yohana alikuwa ndiye Eliya, wa siku hiyo, ambaye alikuwa aje.

73 Sasa, pia tunajua ya kwamba Maandiko wakati mwingine humaanisha mambo mawili. Litasema jambo moja, kama vile pale katika Mathayo ambapo lilisema, "Kutoka Misri nilimwita Mwanangu." Vema, ninaamini hilo ndilo nililokuwa nikitafuta, "Kutoka Misri nilimwita Mwanangu." Halafu kama utafuatilia marejeo hayo ya "mwana" pale, Yeye alikuwa . . . halikuninii . . . lilirudi katika Hosea, ambalo halikumaanisha *Yesu,* Mwana Wake; lilikuwa—lilikuwa Israeli, mwana Wake, "Kutoka Misri Yeye alimwita Israeli." Lakini lilikuwa na maana maradufu na ufahamu mkuu zaidi wakati lilimaanisha na kuzungumza juu ya—ya kuja kwa Yesu, ambaye alikuwa ni mkuu kuliko—kuliko Israeli, wakati alipowaita Israeli watoke. Vema.

74 Sasa, pia tunaona hilo lime . . . katika kuja Kwake mara ya kwanza haikuwa ni Siku ya Bwana. Hiyo ni kweli? Sasa, turudi kwenye Malaki, hebu tulinyoshe hili kwanza, "Kuja kwenye ile Siku ya Bwana." Sasa, angalieni kuja Kwake mara mbili, kule kuja Kwake kumoja na kuja Kwake mara ya pili. Mna mawazo yenu ya kiroho tayari? Kifungu cha 6 sasa, "Ataninii . . . "

. . . . Yeye *atawapelekea . . . Eliya . . . kabla . . . haijaja siku ile ya BWANA, iliyo kuu na kuogofya:* (Hiyo ni kweli?)

75 Sasa, tunatambua ya kwamba huyo hakuwa Yohana, maana haikuwa ni ile Siku ya kuogofya ya Bwana (sivyo?), na Yeye . . . wala hakuiteketeza dunia. Kwa hiyo hapana shaka ilimaanisha utangulizi, ama—ama kuja kwingine usoni kwa Yohana . . . ama kwa—kwa Eliya. Hiyo ni kweli? Maana Yeye alisema, "Nitawapelekea Eliya, nami nitaiteketeza dunia nzima, nami nitaisafisha kabisa, nanyi mtatembea juu ya majivu yao." Hiyo ni ule Utawala wa Miaka Elfu, tunajua hilo. Baada ya bomu la

atomiki kuulipua vipande-vipande, ndipo kutakuwako . . . dunia itanyoka. Ndipo kutakuwako na Siku iliyo kuu hapa duniani, nalo Kanisa litatawala pamoja na Yesu duniani kwa miaka elfu moja. Hiyo ni kweli? "Lakini kabla ya ile Siku ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya, wakati itakapolipuliwa, nitawapelekea Eliya nabii." Hiyo ni kweli? Kwa hiyo haikumaanisha Yohana Mbatizaji katika hali hiyo, kwa sababu ile Siku ya Bwana ya kuogofya haikuwa ni wakati huo, umbali wa miaka elfu mbili. Hiyo ni kweli?

76 Sasa, angalieni kifungu kinachofuata. Ndipo endapo mtakuwa wa kiroho kweli sasa; sasa, hii ni barua ya upendo, nanyi mnapewa kusoma katikati ya mistari na ndipo inafanywa sawa. Mnajua ninalomaanisha. Kumbukeni jinsi nilivyosema, Maandiko, "Yesu alimshukuru Mungu kwa sababu aliyaficha kutoka kwa wenye hekima (wa macho) na maarifa, akawafunulia watoto wachanga." Sasa, mara nyingi nimetoa mfano wa mke wangu wakati anaponiandikia barua; ninaweza kuona yale anayosema kwenye barua, bali ninasoma katikati ya mistari kujua yale anayomaanisha, mnaona, kwa maana ninampenda na mimi—mimi najua tabia yake. Nawe huna budi kuijua tabia ya Mungu na kumpenda, ndipo Maandiko yanadhihirika wazi wazi kwako. Yeye anayafunua.

77 Sasa, angalieni kifungu kifuatacho:

> *Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao,* (Sasa, angalieni.) *na* mioyo *ya watoto iwaelekee baba zao* . . . (Mnaona?)

78 Sasa, wakati Yohana alipokuja kama Eliya, aliigeuza mioyo ya Waisraeli, mioyo ya watoto ambao wakati huo walikuwa wakiukubali ujumbe wake, mioyo ya baba iwaelekee watoto. Lakini anapokuja wakati *huu*, yeye ataigeuza mioyo ya Kanisa iwaelekee baba wa Kipentekoste. Mnaona, ni vinginevyo hapo. Mnalipata? Sasa, lisome!

79 Sasa, sikilizeni kwa makini sasa:

> *Naye ataigeuza* mioyo *ya baba iwaelekee watoto wao,* . . .

80 Yule kuhani wa kale wa kiorthodoksi; yeye atawaambia ya kwamba, "Mbona, Mungu anaweza kwa mawe haya hapa kumwinulia Ibrahimu watoto. Hivi hamfikiri kwamba mnaweza . . . " Mnaona? Sasa, yeye ataichukua mioyo ya maskini kuhani wa kiothodoksi asiyejali na kuigeuza mioyo yao ielekee kwenye Imani ambayo watoto hawa walikuwa nayo hapa. Mnaona, "Sasa, wote hawa ambao wamebatizwa na wanakungojea kuja kwa Masihi. Ni nani aliyewaonya, enyi uzao wa nyoka, kuikimbia hasira ijayo?" Loo, jamani! Mnaona, "Alikuwa akiigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto."

81 "Na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao." Sasa, Eliya *huyu* mkuu atakapokuja mwishoni mwa wakati huu, atakuwa

akiuchukua Ujumbe wa Kipentekoste kuwageuza watoto waelekee kwenye Imani ya wale baba zao, kwa sababu atakuwa akiwakemea kwa sababu hawakudumisha Imani ii hii iliyokuwa huko nyuma mwanzoni. Amina! Sasa, ninaamini tunatambua vizuri sana kwamba itakuwa ni Eliya. Sivyo? Sasa tunajua hilo.

82 Na imekuwa . . . Sasa mnaona, Siku ya kuogofya ya Bwana haijaja. Mara nyingi nimeshangaa, "Je, mtu huyu atakuwa tu ni mhubiri, basi?" Eliya alifanya miujiza yote, hakuhubiri. Lakini wakati Roho yake ilipokuwa juu ya Yohana, ilifanya mahubiri yote pasipo na miujiza. Kwa nini? Yesu alikuwa amfuate, Yeye angefanya miujiza, "Kwa kuwa Jua la haki litawazukia," yeye alisema, "lenye kuponya katika mbawa zake." Kwa hiyo Yohana hakuwa na haja ya kufanya miujiza, yeye alitangaza tu kuja kwa Kristo. Nao hao . . .

83 Sasa, kumbukeni, basi Yohana huyu . . . ama Eliya huyu atakayekuja, atafahamika vibaya, yeye atakuwa mtu mwenye nguvu sana mbele za Bwana mpaka watu watafikiri yeye ni Masihi.

84 Kwa sababu marafiki zake walio wazuri sana walimwambia, "Wewe ndiwe Masihi."

85 Yeye alisema, "Mimi sistahili kuvifungua viatu vyake, bali anakuja baada yangu!"

86 Kwa sababu walikuwa chini ya matarajio, basi, kumwona Masihi, walidhani Masihi alikuwa anakuja . . . Wakati walipoona jambo hili kuu likizuka miongoni mwao, walisema, "Yeye ni Masihi."

87 Yohana alisema, "Mimi si Yeye! Lakini anakuja baada yangu!"

88 Loo, jamani! Mnalipata? Kwa hiyo marafiki zake wa karibu watafikiri yeye ni Masihi.

89 Sasa, angalieni jambo lingine litakalotukia, tabia ya hili, yeye atakuja kabla tu ya ile Siku ya Bwana. Sasa, dunia haikuteketezwa katika siku za Yohana, kwa hiyo iko katika siku za usoni. Wakati alipokuja mara ya kwanza, yeye alihubiri tu; mara ya pili, yeye—yeye atahubiri na pia kufanya ishara zilizoahidiwa na Yesu Kristo. Vema, sasa, hebu tuangalie ile tabia, itakavyokuwa, tabia ya nabii huyu ajaye.

90 Sasa, tumeridhika ya kwamba malaika wa wakati huu wa mwisho wa kanisa, aliyetabiriwa kutoka kwenye Agano la Kale na kuendelea; sasa, hao wengine hawakubashiriwa. Paulo, Ireneo, hawakubashiriwa. Lakini wakati huu wa mwisho, mwisho wa ukamilifu wa dahari, mwisho wa ulimwengu, utakuwa ni wakati wa ajabu sana tulio nao mbele zetu, kwa hiyo malaika huyu wa wakati huu alitabiriwa huko nyuma kabisa katika Maandiko, Maandiko ya Kale, mwisho wa wakati huu. Ni Eliya, mtu mkuu aliyepakwa mafuta.

91 Sasa, angalieni! Eliya atakuwa na tabia ya aina gani? Kwanza, atakuwa nabii mkuu aliye mwaminifu kwa Neno la Mungu, kwa kuwa Eliya alikuwa mkweli, naye Yohana alikuwa mkweli. Hiyo ni kweli. Akifanya ishara na maajabu, ataigeuza mioyo ya watoto iirudie Imani ya baba wa Kipentekoste. Atayachukia madhehebu kama Eliya alivyofanya. Hiyo ni kweli, atayachukia! Nafikiri tumekianzisha kitu hicho kwa ajili yake sasa; wakati wa kuja kwake umekaribia. Atayachukia madhehebu! Eliya aliyachukia, na vivyo hivyo Yohana aliyachukia madhehebu.

92 Yohana alisema, "Msije, msiwazie, 'Sasa tuna Ibrahimu baba yetu.' Enyi Mafarisayo na Masadukayo, enyi kundi la nyoka! Nyoka nyasini," kwa maneno mengine. "Kwa maana nawaambia, Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto."

93 Eliya alisema, "Wote wamepotea, kila mmoja wao! Hakuna aliyesalia ila mimi peke yangu." Loo, jamani!

94 Yeye pia atawachukia wanawake waliojipamba! Eliya aliwachukia: Yezebeli. Hiyo ni kweli? Yohana aliwachukia: Herodia. Manabii wote wawili, Roho, Roho ile ile. Waliuchukia ulimwengu wa kimadhehebu, ulimwengu wa kikanisa. Waliwachukia, pia, wanawake wabaya, waliojipamba. Wao... Kitu fulani ndani ya roho yao kilikikemea sana kitu hicho! Yezebeli alikuwa akikitafuta kichwa cha Eliya na alikuwa akitaka kukikata; naye pia alifanya kichwa cha Yohana kikatwe, Herodia alifanya. Wote wawili!

95 Nabii huyu atakuwa mpenda nyika! Kama Eliya, Yeye aliishi nyikani, peke yake. Yohana, nyikani, peke yake. Basi tunajua itakuwa ni Eliya. Vema.

96 Naye nabii huyu atakuwa ambaye atadumu na Neno la kweli la Mungu. Naam, atadumu Nalo, Neno lote. Kufanya nini? Kuirejesha Imani (kwenye kanisa la Efeso) iliyokuwa imepotea wakati huu wote, Imani, katika kanisa lililokuwa na "Mlango uliofunguliwa" uliowekwa mbele yake nalo likaukataa.

97 Sio mtu mwenye elimu. Eliya hakuwa ni mtu mwenye elimu, yule Mtishbi. Yohana hakuwa mtu mwenye elimu. Luka 1:67, Biblia ilisema ya kwamba alikuwa..."Kwamba mtoto huyo alikuwa katika...mara alipozaliwa, alienda nyikani, alikuwa nyikani mpaka siku alipotambulishwa kwa Israeli." Hiyo ni kweli. 1:...Luka 1:67 hadi kifungu cha 80, kama mkitaka kukiandika.

98 Nabii huyu pia atakuwa jamaa mwenye hali ya vipindi vya kusononeka. Eliya, baada ya kufanya mkutano mkubwa, hakuna mtu angaliweza kusikilizana naye. Eliya alikuwa na vipindi. Wakati alipotoka akaenda huko nje na kuagiza moto kutoka mbinguni na kuyateketeza madhabahu ya Baali na kila kitu, yeye alikimbia huko nyikani na kusema, "Bwana, mimi si bora

kuliko baba zangu, acha nife." Hiyo ni kweli? (Naye Yohana . . .) A—aliketi chini ya mretemu, na baada ya ule uamsho mkuu, sasa alitaka kufa.

99 Naye Yohana, walipomtupa gerezani (mwanamke huyu mwovu) aliketi kule nyuma na kuanza kuingiwa na hali ya kusononeka. Ninaamini Pember ama mmoja wao alisema, "Jicho lake la tai liliingia utando, gerezani." Akatuma baadhi ya wanafunzi wake.

100 Na, mbona, alikuwa ametangaza, kasema, "Yule pale Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu." Yohana aliona ile Nguzo ya Moto ikining'inia juu Yake, kama Hua, kisha ikashuka, ikakaa juu Yake. Alishuhudia yote, na kusema, "Huyo ni Mwana-kondoo wa Mungu!" Kisha kasema, "Nina haja ya kubatizwa na Wewe, basi mbona waja kwangu?"

Yesu akasema, "Kubali iwe hivyo sasa."

101 Lakini wanapomweka gerezani, anadhoofika upesi sana. Mnaona, kwa namna fulani ni ngumu, ni vigumu kumwinua. Nao walipofanya hivyo, alisema, "Nendeni mkamwulize kama Yeye kweli Ndiye, ama tumtazamie mwingine?" Kama tu Eliya alivyofanya hasa, mnaona, vile vile tu.

102 Yeye, kwa namna fulani mtu anayeshikwa na sononeko, kwa hiyo tunamsikitikia maana tunajua kile hiyo ilicho. Vema.

103 Sasa, sasa kwenye . . . Ka—Kanisa, kwenye kudhihirishwa kwake . . . Afadhali niachane na hilo. Katika kudhihirishwa kwake, Ka—Kanisa . . . Atakapojitambulisha, Eliya huyu mwenye nguvu ambaye Mungu atatutumia, wakati atakapojitambulisha kama Eliya alivyofanya, Kanisa lilikuwa tayari kukombolewa, lilikombolewa kutoka kwenye mikono ya upagani. Hiyo ni kweli? Mara tu alipokuja kule juu na kusema, "Tutathibitisha Mungu ni nani," Eliya alililikomboa Kanisa. Naye Yohana, kama tu alivyofanya Yohana, yeye alisema wakati alipomwona Yesu, alisema, "Sina budi kupungua Naye hana budi kuzidi." Yohana alianza kuhubiri, akajitambulisha kabla tu ya kule kuja kwa Bwana. Moja kwa moja mwishoni, lile dhihirisho. Vema.

104 Sasa, tunaona ya kwamba Eliya hana budi kumaanisha wakati huu kwa Kanisa hili. Kuthibitisha ya kwamba ilikuwa ni Eliya: Eliya akiisha kuutoa unabii wake, Eliya haikumbidi kufa, yeye alihamishwa na akatwaliwa juu Mbinguni; mfano wa Kanisa (mwishoni mwa Eliya huyu atakayekuja, mwishoni mwa wakati *wake*), Kanisa litaingia katika Unyakuo, pasipo kupitia kwenye uvuli wa mauti. Itakuwa ni ule Unyakuo! Ninaamini yule Eliya mkuu, yule mkuu anayepaswa kuja, atakuwa ni Eliya aliyetiwa mafuta ambaye ametabiriwa kwa ajili ya siku za mwisho. Amina! Nafikiri atakuwa, hapo atakapokuja, yule malaika, ama mjumbe wa kanisa katika siku za mwisho (watu waliokataliwa, waliovunjiwa heshima, kama vile kanisa hili

litakavyofikia, na liko tayari). Nafikiri Eliya ameahidiwa katika Biblia. Nafikiri tunaweza kuelewa hilo, ya kwamba Eliya ndiye aliyeahidiwa katika Biblia kuja katika siku hii. Mnaamini hilo?

105 Sasa hebu tugeukie Laodikia sasa ndipo tutaona yale Bwana wetu atakayotwambia usiku wa leo kuhusu Laodikia, Laodikia fulani. Vema, salamu kwa kanisa:

> . . .*kwa malaika wa* Bwana . . .

106 Kifungu cha 14 kwenye mlango wa 3 wa Ufunuo:

> . . .*kwa malaika wa* Bwana . . .*wa* . . .*Laodikia andika; Haya* ndiyo *asemayo yeye aliye Amina, shahidi aliye mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu;*

107 Loo, jamani! Tuna ninii yote . . .Kama tulikuwa na usiku kucha kwenye hayo papo hapo, jinsi ambavyo Bwana angetufunulia hayo! Angalieni!

108 Yule "Amina" ni wa "Mwisho." Ameonekana kote kote, na vitu mbalimbali, bali huu hapa wakati wa mwisho wa kanisa ambapo linasema, "Mimi . . .Huku ni kumalizia, Mimi ndimi wa Mwisho."

109 Sasa, kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni wa "Kwanza" pia, kama alivyokuwa, Yeye ni "mwanzo wa uumbaji wa Mungu." Loo! Mnalipata? Mnaona? Mungu angewezaje kuumbwa kama Yeye ni Roho? Angewezaje? Yeye—Yeye ni wa Milele! Hakuumbwa kamwe, kamwe hataumbwa, kwa sababu Yeye alikuwa ni Mungu hapo mwanzo. Bali Yeye aliye "mwanzo wa kuumba kwa Mungu" alikuwa ni Yesu Kristo alipodhihirishwa, hapo Mungu alipoishi ndani Yake. Yeye ni *uumbaji* wa Mungu! Loo, jamani! Mnaona, "Wa Kwanza na wa Mwisho; Amina, mwanzo wa kuumba kwa Mungu." Wakati Mungu alipojiumbia Mwenyewe mwili, Yeye alishuka na kuishi ndani yake, huo ndio mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Mnaona? Loo, Yeye si ni wa ajabu?

110 Sasa, tunaona hapo mwanzo, Yeye aliuonyesha Uungu Wake papa *hapa*, "Mimi ndimi Mwenyezi! Mimi ni Yule Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja. Mwenyezi!" Kwa kanisa la Efeso, alisema mara tatu. Hiyo ni kweli? Akaja moja kwa moja kwa Laodikia na kusema, "Mimi ndimi Amina. Nilikuwa wa Kwanza *hapa* nyuma, Mimi ni wa Mwisho *hapa*. Nami ndimi mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Kupitia kwa nyakati za kanisa ambazo tunapaswa kuwa nazo, mtajua ya kwamba Mimi ni Mungu, Mungu aliyeumbwa kwa mfano wa mwanadamu. Mimi ndimi mwanzo wa kuumba kwa Mungu!" Amina.

111 Hilo lingemfanya Mpresbiteri apige makelele. Liwazie tu! "Mwanzo wa kuumba kwa Mungu." Sasa, mimi . . .Loo, jinsi ninavyolipenda hilo, "kuumba kwa Mungu," wakati Mungu

alipoumbwa, wakati Mungu alipofanyika mwili katika Yesu Kristo na kukaa miongoni mwetu.

112 Sasa—sasa, kifungu kinachofuata kingekuwa (kwa makanisa hayo mengine) kuyasifu, bali Yeye hakulisifu kanisa hili. Alikuwa na malalamiko dhidi yake, sio sifa. Hakulisifu hili kwa chochote, wakati huu wa Laodikia. Pamoja na Nuru yote waliyokuwa nayo, nao wakaiacha, hawakuhitaji sifa zozote. Ah-huh. Walihitaji kemeo, nao wakalipata! Alikuwa na malalamiko juu ya kanisa hili, si sifa.

113 Sasa ninataka kusoma kifungu cha 15 na cha 16 hapa sasa:

> *Nayajua matendo yako,. . .hu baridi wala hu moto: ingekuwa heri* kama *ungekuwa baridi au moto*. (Kwa maneno mengine, "Usi—usiwe tu vuguvugu.")
>
> *Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu.* (Hmm!)

114 Kufundisha. . .Hizo ni sifa? Hilo ni kemeo kwa wakati huu mwovu wa Laodikia, ulio mbaya sana wa kundi hilo zima. Huo mwingine wote chini ya mateso na kila kitu walichokuwa nacho. Hawakuwa na kitu, walikuwa maskini hohehahe, walitangatanga wamevaa ngozi za kondoo na za mbuzi, na fukara, wakakatwa kwa misumeno na kuchomwa moto hata kufa, wakalishwa kwa simba, na kadhalika, na hata hivyo bado waliishikilia Imani. Nalo kundi hili ni "tajiri wala hawana haja ya kitu," na kila kitu kingine, na ni kahaba! Hiyo ni kweli.

115 Sasa, tuna somo kubwa mno, ninatumaini Bwana atatusaidia. Yeye—Yeye alisema, "Kwa sababu hu baridi wala moto, vuguvugu."

116 Kama vile maziwa, mnaona. Maziwa mazuri baridi ni mazuri. Sivyo? Maziwa moto ni mazuri kwako. Lakini maziwa vuguvugu yatakufanya utapike.

117 Nakumbuka usiku mmoja nilikuwa mgonjwa, huko chini mtoni, yapata miaka ishirini na mitano iliyopita. Nilikuwa katika kibanda kidogo cha mtumbwi, nikiishi kule chini. Nikawa mgonjwa, nao wakaja, shemeji yangu alikuwa amenipeleka kwa Dk. Isler. Kasema, "Kwani kuna nini?"

Nikasema, "Ninaumwa sana na tumbo langu!"

118 Kasema, "Kunywa bilauri ya maziwa yenye joto." Loo, ndugu! Maziwa yenye uvuguvugu, yalinichefua, kwa hiyo nikayatapika yote yaliyokuwa ndani.

119 Sasa, Mungu alisema, "Afadhali ungekuwa moto, moto kabisa, ama kuganda kwa baridi, uwe mmoja ama mwingine. Usiingie uvuguvugu, maana unanichefua."

120 Hivyo ndivyo wakati huu wa kanisa unavyomfanyia Mungu, unamchefua! Mnaona? "Ama uwe. . . Usi. . . Am-. . . usiwe ninii. . . Ama uwe moto kabisa au. . . Usiwe vuguvugu! Vuguvugu ama joto; maana unanifanya nitapike."

121 Ubaridi wa kanisa la Kianglikana katika siku za John Wesley ulimsukuma akafanyie mikutano mahali pengine, kwa kuwa lilikuwa baridi, limeganda.

122 Ubaridi wa kanisa la Kimethodisti ulimfanya William Booth kuwa mwana-wokovu motomoto sana. Mnaona, Mungu alisema, "Msipokuja na kutubu, nitakiondoa kinara cha taa. Nitakitoa, nimpe mtu mwingine." Kwa hiyo wakati kanisa la Kimethodisti lisingeupokea utakaso wa John Wesley, William Booth alikuja moja kwa moja pamoja na Jeshi la Wokovu na kulisongesha mbele. Hiyo ni kweli. Kwa nini? Waliliundia dhehebu! Hiyo ni kweli kabisa. Wakaunda dhehebu kutoka kwake, ndipo Mungu akasema, "Nakichukia kitu hicho!"

123 Kwa hiyo ninii. . . William Booth alikuja moja kwa moja na kulichukua, na Jeshi la Wokovu, ndipo akafanya nini? Jambo lile lile, wakageuka na kuliundia dhehebu tena. Baada yake wakaja Wakampbeli, nao wakadumu kwa muda kidogo; kisha John Smith na Wabaptisti; ndipo baada ya hao wakaja Wanazarayo; halafu baada ya Wanazarayo ikaja Pentekoste.

124 Wanazarayo, wangefanya nini? Wakalitengeneza lao vivyo hivyo, wakaliundia dhehebu.

125 Ni kitu gani kilichotokea wakati huo? Matawi mawili madogo, Church of God na kadhalika, yalichipukia kutoka hapo. Walifanya nini? Wakaunda dhehebu; akawaachilia tu.

126 Moja kwa moja wakaja Wapentekoste wakiwa na baraka za mvua ya vuli, walifanya nini? Wakaunda dhehebu, kwa hiyo Yeye akawaachilia tu. Hiyo ni kweli.

127 Sasa tutafikia hapa mwishoni, mpate kitu chenye nguvu kweli katika dakika chache. Vema.

128 Vema, Yeye anakutaka moto kabisa ama—ama umeganda kwa baridi, moja au jingine. Usiwe vuguvugu! Kamwe usijifanye una kitu usicho nacho, ama uwe unawaka moto kwa ajili ya Mungu ama uende huko nyuma kwenye—kwenye—kwenye dhehebu. Usi—usiwe vuguvugu!

129 Ni jambo lile lile sasa! Hilo ni jambo lile lile lililotukia katika. . . makanisa haya hapa. Anakutaka ama uwe moto au baridi. Hataki "uvuguvugu" wowote. Hapo ndipo Pentekoste imefikia, hali ya uvuguvugu. Wanaenda kwenye piano mara moja moja, na ngoma chache, nao wanagonga-gonga kidogo; nao wanapata muziki wa kutosha, mtu fulani anasimama na kwa namna fulani. . . mwajua, kwa namna fulani anasema, "Bwana asifiwe! Haleluya!" Uh-huh. Kisha muziki unashuka, "Uh,

Uhu, uhu, *uhu*," kwisha. Loo, jamani, linamfanya tu Mungu kuchefuka tumboni Mwake! Mnaona? Uh-huh. Vema.

130 Hakuna mengi yanayoendelea basi, wakati—wakati uamsho motomoto ukiendelea ndani yao, bali walikuwa na mitambo mingi ya kimashine katika kanisa hili, mnaona, maana walikuwa tajiri na, loo, jamani, walikuwa wakija pamoja na kufanya mikutano mikubwa na kadhalika. Walikuwa na wakati mzuri katika kanisa hili, hiyo yote ni kweli, bali yote ilikuwa ni mitambo ya kimashine. Bali hakuna lile joto la Roho Mtakatifu. Mnaona?

131 Angalieni hapa yale Yeye aliyosema hapa, mnaona:

> *Nayajua matendo yako,. . .wewe* hu *baridi wala hu moto: ingekuwa heri kama* wewe ungekuwa *baridi au moto.*
>
> Basi, *kwa sababu* una *uvuguvugu,. . .hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu.* (Mnaona?)

132 Sasa, Yeye alisema, "Ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Na kwa kuwa sivyo ulivyo, si—sina budi tu kukuondosha, hivyo tu, nikutoe tu kinywani Mwangu."

133 Sasa, walikuwa na fedha nyingi sana, walikuwa na majengo makubwa, walikuwa na mambo makuu yakiendelea, bali hawakuwa na joto la Roho Mtakatifu. Loo, walikuwa na mita-. . .shi—shirika. Loo, jamani! Walifanya Muungano wa kanisa. Jamani, walipata jengo kubwa sana walilopata kuwa nalo, na mambo yakiendelea, bali bila ya Roho Mtakatifu. Mnaona? Huyo ndiye Mungu aliyelitumia Kanisa, Roho Mtakatifu.

Sasa, tunapoendelea na kifungu hiki cha 16.

134 Wana kila namna ya kamati. "Loo, tuna shirika kubwa la hilo. Shirika la misaada la mama wazee, na—na mchezo wa pinochle wa vijana, na—na mchezo wa karata Ijumaa usiku, na mchezo wa vi—vikapu Jumapili alasiri, na, loo, mchezo wa besiboli siku *fulani-fulani*. Na, loo, ndio kwanza tuunde shi—shirika la kupiga domo la wanaume. Na, loo, tuna mambo ya kila namna."

135 Nawaambia, limelemewa na mizigo, mashirika, na vilabu, na kupigwa, na chochote kile, bali hamna joto la Roho Mtakatifu. Mnaona, mna shirika kubwa, bali hamna kitu hapo cha kuwapasha joto. Mnapata joto la ulimwengu bali si la Mungu, hiyo ndiyo sababu ninyi ni vuguvugu.

136 Loo, mna wafuasi wengi kuliko mlivyopata kuwa nao. "Hakika, jamani! Mbona, tulipata milioni moja zaidi katika mwaka wa '44," lasema Baptisti. Lakini—lakini una nini? Mtambo mkubwa!

137 Moja kwa moja kwenye kanisa lilo hilo nilimosikia tamshi hilo likitolewa, iliwabidi kupumukana dakika kumi na tano, kumpa mchungaji nafasi ya kutoka nje, na mashemasi wote na hao wengine, kuvuta sigara, kisha warudi tena. Mnaona? Haya basi. Biblia inahukumu hilo kwa udhahiri sana! "Ukiutia mwili huu najisi . . . "

138 Madaktari wanaihukumu hiyo na kusema, "Imejaa kansa." Halafu wanaingia kwenye redio na kusema, "Chujio la mtu mwenye busara."

139 Kama Billy Graham alivyosema, "Yeye ni mpumbavu kuwazia hilo kwanza."

140 "Chujio la mtu mwenye busara," mtu *mwenye busara* asingeivuta hata kidogo, hiyo ni kweli, unachukua wazo la pili. Lakini anawaambia wanawake inawafanya wembamba sana, mwajua, kusudi waweze kuvaa baadhi ya hizi nguo mpya walizo nazo. Jamani, hilo linaziuza! Wanawake wengi zaidi wanavuta sigara kuliko wanaume sasa, naye mwanamke atavuta sigara tatu kwa moja, kwa mwanamume. Hiyo ni kweli kabisa, maana anataka kuwa mwembamba. Hatambui hiyo ni TB na kansa na kadhalika inayomfanya hivyo, katika hali tu ya uchanga, ikiingia ndani yake, ikimla namna hiyo, ikimwua. Hakuna kitu kinachoweza kutoka kwake ila uovu! Hiyo ni kweli. Mnaona? Lakini hilo ni, "Ni—ni chujio la mtu mwenye busara." Hah! Loo, jamani!

141 "La! La! Loo," wao wanasema, "lakini tuna ninii . . . Ndugu Branham, ninakanusha hilo! Tuna mikutano mikuu! Angalieni yale Billy Graham amekuwa nayo kote nchini." Loo, hakika, shirika kuu, wainjilisti waliokodishwa, viongozi wa nyimbo wanaolipwa.

142 Naam, wanawakodi wainjilisti wao. "Vema, utanilipa kiasi gani kama nikija na kuufanya uamsho huo? Vema, kama huwezi kutoa *kiasi hiki* cha maelfu ya dola sitakuja kamwe. Hiyo ni kweli. Basi ni nani mtakayemruhusu kuongoza uimbaji? Vema, nenda ukamkodi *Fulani-wa-fulani*, yeye ni mwimbaji hodari wa solo. Ukimlipa kuninii . . . Yeye atavutia nusu ya umati wangu, atauvutia mwenyewe."

143 Solo wa kulipwa! Wainjilisti wa kulipwa! Mbona, imefikia mahali ambapo kuwaokoa watu ni biashara. Kuokoa nafsi si biashara ya kanisa, ni nguvu za Roho Mtakatifu kanisani. Kuokoa nafsi si . . . huununui kwa fedha. La, bwana! La! Yote ni, ni kazi, kazi, kazi, wainjilisti wa kulipwa, viongozi wa nyimbo wa kulipwa, kwaya za kulipwa, kila kitu kingine. Mungu hataki hivyo, yote ni kazi! Mungu hataki kazi, anataka Roho Mtakatifu akifanya kazi ndani yenu. Hiyo ni kweli.

144 Kifungu cha 17 kinasema:

> *Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri . . . nimejitajirisha, wala sina haja* ya *kitu; nawe hujui ya kuwa wewe*

> *ni mnyonge,* (Loo!)*. . .hujui ya kuwa wewe ni mnyonge,. . .mwenye mashaka,. . .maskini,. . .kipofu, na uchi:* (Hmm! Hmm!)

145 Walidhani walikuwa ni "tajiri," Pentekoste hii katika makanisa haya ya wakati wa mwisho. Walidhani. . .Na kwa nje walikuwa. Naam, bwana. Wao ni matajiri. Wazia tu kanisa, ilikuwa miaka michache iliyopita, lilisimama kule pembeni, likitupwa mahali mahali, lilikuwa na wakati mgumu. Lakini sasa yana baadhi ya mijengo mikubwa sana iliyopo.

146 Mnaona ambapo Assemblies of God hapa nje, waliokuwa na mahali pao katika jengo la kawaida la mbao, kitu kama hiki hapa, na sasa wanajenga jengo la dola milioni sita, nao wanasema, "Yesu yuaja mara moja." Kazi zenu zinathibitisha ya kuwa hamuamini hilo. Ni unafiki! Kujenga mijengo ya dola milioni moja na mambo kama hayo, na kusema, "Yesu yuaja mara moja." Na maskini wamishenari wakiwa hudumani, bila viatu miguuni mwao, wamishenari wacha Mungu kwelikweli, bila viatu miguuni mwao, huku wanaishi kwa vipimo viwili vya mchele kwa juma; wanakula mara mbili kwa juma wapate kuipeleka Injili misituni na mambo kama hayo, kuipeleka kwa ndugu zao. Nasi tunajenga mijengo ya dola milioni sita, na kanisa lenye madirisha makubwa ya vioo vya rangi, na kila kitu kingine, na kuiweka kwenye hilo. Loo, hata mna fedha nyingi sana mpaka wakati mwigine wana mashirika ya mikopo mumo humo makanisani. Hiyo ni kweli!

147 Daktari humo ndani kuwachunguza wainjilisti wao ama wamishenari wao. Na mtu akitaka kwenda hudumani, wanamfanyia uchunguzi wa daktari waone kama yeye. . .ama mtaalamu wa akili, waone kama yeye. . .loo, kama IQ yake iko sawa kiakili, mnaona. Roho Mtakatifu huzichunguza hizo, humhitaji mtaalamu wa akili.

148 "Lakini, sisi ni tajiri na hatuna haja ya kitu." Loo, hakika. Mna pesa nyingi sana. Kwa nje, matajiri sana; mna mijengo mikubwa, madirisha ya rangi.

149 Na wahubiri wenye lugha ya ushawishi! Loo, jamani. Jamani, nitawaambia, hmm, hao wana ushawishi kweli. Wanaweza kusimama na kuzungumza usiku kucha, na wasiseme kitu. Mnaona? Wanapokuja. . .Ninamaanisha kuhusu mambo wasiyopaswa kusema, mnaona. Kusimama, na baadhi ya upuuzi huu, na kuzungumza kuhusu maskini *hiki-na-hiki* na *hiki-na-hiki*. Nanyi mwajua jinsi ilivyo. Waimbaji wa kulipwa. Hiyo ni kweli. Vema. Lakini, wanakuja mimbarani, wahubiri washawishi. Kama hawajavaa suti rasmi pamoja na ukosi uliopinduliwa, na namna fulani ya koti lenye mkia, mbona, kusanyiko lao linajisikia limeaibishwa kweli.

150 Nao hao waimbaji wanajitokeza huko nje, hao wanawake, nywele fupi zilizokatwa kama Yezebeli, wana rangi za kutosha

usoni mwao kupaka rangi kibanda kizima. Mara wanapolivua hilo joho, wanavaa kaptura na nguo za wanaume, nayo Biblia ilisema, "Mwanamke akivaa vazi limpasalo mwanamume, ni chukizo machoni Pake." Wanashuka kwenda mtaani wameinua pua yao, kama kungenyesha mvua ingewazamisha. Mayezebeli wajuaji, wenye kiburi, wenye hasira kali! Hiyo ndiyo sababu hatuko kwenye uamsho wowote, ni kipande kikubwa cha kazi ya mitambo.

151 Loo, huenda wakawa na sauti kama ya malaika mkuu, naye Mungu atawawajibisha kwa jambo hilo! Hawa akina Elvis Presley na kadhalika, na akina Ernie Ford, ama vyovyote waitwavyo huko nje pamoja na sauti hizi nzuri na kuzitumia kwa ajili ya ibilisi, Mungu alisema, "Nitaitaka hiyo mikononi mwao."

152 Hiyo ndiyo sababu ninamheshimu kipofu Fanny Crosby; yeye kamwe hakuiuza karama yake kwa ulimwengu. Aliiweka kwa Mungu.

153 Wengi wa watu hawa ni waimbaji wenye vipaji, watu wenye vipaji, watu mashuhuri, na kadhalika, badala ya kutumia vipaji vyao kwa ajili ya Mungu, ibilisi amewapotosha nao wako kule wakimfanyia kazi. Watu mashuhuri, watu mashuhuri wa redio na televisheni, wakijiuza, huko nje kwa ulimwengu badala ya kumpa Mungu. Baadhi yao huja kanisani, wanaenda kanisani, wanavaa joho kubwa zuri, wanatoka hapo na kuimba namna hiyo, na kurudi moja kwa moja na kuimba roki kesho yake usiku. Waimbaji kama hao tunaowajua, ni wafuasi wa makanisa fulani, wanatoka huko nje na kupiga picha hizo, hizo picha za sinema, wanaenda huko nje na kuimba roki. Wafalme wa roki, na kudai kuwa wa kidini! Ni ujanja wa ibilisi!

154 Mtu mmoja alikuwa na akili timamu ya kutosha—kutosha hapa juu. Aliyesema atakuwa mhubiri, angeenda Jumapili asubuhi na kuhubiri, kisha angeshuka aende kule chini kwenye. . .na kuchukua utangazaji wa redio na kuimba nyimbo za roki na kadhalika namna hiyo, kwa hiyo hatimaye alichukua bastola na kulipua ubongo wake. Ninamheshimu mtu huyo kwa kufanya hivyo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. A—alikuwa na ninii zaidi. . .Alikuwa na akili kadiri ya wale nguruwe walizokuwa nazo, kwa vyovyote vile, wakati walipoingiwa na ibilisi walikimbilia majini wakajizamisha mle. Baadhi ya watu hata hawana kiasi hicho.

155 Ninajua ninyi. . .na—nachukia kuwa mkali hivyo, bali, ndugu, dada, huna—huna budi kushindilia kitu hicho hapa chini kukifanya—kukifanya kishikilie! Hii ndiyo siku tunayoishi. Nadhani kama Yesu alimwita Herode "maskini mbweha," naye Yohana akawaita "kizazi cha majoka," vema.

156 Wana mijengo mikubwa, madirisha ya rangi, wahubiri wenye ufasaha wa lugha, waimbaji wa kulipwa. Naam, bwana. Wana nini ndani yake? Kina nini? Hakuna kitu cha Roho

Mtakatifu. Wanasimama pale kisha wanatoka na kuvaa kaptura, halafu wanaingia na kuimba katika kwaya. Ewe mnafiki mwenye mashaka! Naam, bwana. Hiyo ni kweli.

157 Nawe, mhubiri, ambaye utaenda mkutanoni kwa sababu wanakupa pesa nyingi kuliko wanavyofanya mahali pengine! Mhuni wee, hustahili kuwa mimbarani. Hiyo ni kweli. Pesa! "Kama huwezi kutoa dola elfu *kadhaa*, vema, hatuwezi kuja. Ma—ma—mameneja wetu na kadhalika watakuja huko, ikiwa unaweza kupata pesa tutakuja. Kama siwezi kupata ushirikiano mkamilifu na kila mtu, sitakuja. Kama kila mtu hatashirikiana kikamilifu (makanisa yote) kusudi nipate pesa nyingi sana kulipia madeni yangu, sitakuja."

158 Ndugu, mtu halisi wa Mungu angeenda ikiwa Roho Mtakatifu alimwongoza, haidhuru kulikuwa na nini kwenye matoleo. Hata kama ilimlazimu kula biskuti kavu na kunywa maji ya umande. Hiyo ni kweli, yeye ni mtumishi halisi wa Mungu.

159 Lakini watu wanajifunga kwa matangazo na redio na televisheni, na kila namna ya mambo ya ulimwengu, mpaka inawabidi kuwa na fedha kama hizo. Hiyo ni kweli kabisa. Mnaona? Huyo si Mungu.

160 Yeye alisema, "Loo, wewe ni tajiri, huna haja ya kitu." Hakika, bali kile kitu chenyewe ulichohitaji, hukuwa nacho. Hiyo ni kweli. Bali hukukijua. Mnaona, "Tajiri, huna haja ya kitu." Wanalipwa kufanya mambo wanayofanya, kucheza kamari. "Loo," mnasema, "tuna makusanyiko makubwa." Loo, hakika. Naam, bwana. "Kusanyiko kubwa kuliko yote! Mbona—mbona, unajua, meya wa mji huu huja kanisani mwetu." Um-hum. Hiyo ni kweli. "Vema, wajua, *Fulani-wa-fulani,* wanapokuja mjini, wanakuja kanisani mwetu." Um—hum. "Watu wote mashuhuri wamo kanisani mwetu."

161 Naam, na hebu maskini, watakatifu wahitaji waje kanisani, nao ni kemeo kwenu. Hata hamuwataki huko. Mnahofia mtu fulani atasema "Amina!" wakati mkihubiri.

162 Kama vile maskini mama yule niliyesoma habari zake katika kitabu kidogo hapa juu, yeye alikuja kanisani. Watoto wake, alikuwa amewalea katika kanisa la mtindo wa kale huko mwituni mahali fulani ambako walikuwa ni watauwa kweli. Kwa hiyo ninii. . .Jamaa mdogo aliingia siku moja na kumwoa huyo msichana. Kasema yeye ni mfuasi wa kanisa la *nje*, mwajua, moja ya makanisa makubwa ya dhehebu lile lile huko mjini. Kwa hiyo akamwambia huyo mama yeye alikuwa ni Mkristo. Kwa hiyo akamwoa huyo binti na kumpeleka huko nje.

163 Vema, hatimaye akamwondoa kwenye tabia za maskini lile kanisa la mashambani huko nyuma milimani, huku nje, kanisa hili kubwa mno zuri, jina lile lile; ila huko nyuma walikuwa na

Roho Mtakatifu, huku nje hawakuwa na chochote. Kwa hiyo basi wakati walipoingia, kanisa hili kubwa zuri.

164 Kwa hiyo Mama akasema, siku moja, alikuwa akishuka kuja ku—kumwona bintiye. Vema, hawakujua kabisa wangefanya nini naye. Kwa hiyo alipokuja alionekana kama kitu fulani kutoka kwenye vitabu vya kale, moja ya hizo maskini nguo zenye shingo ndefu, mwajua, na mikono mirefu, na nywele zake zimesokotwa huko nyuma, uso laini kama kitunguu, namna hiyo (kimemenywa kuelekea nyuma, mwajua). Ndipo akashuka akaja, naye akasema, "Vema, Haleluya, kipenzi! Nyote mnaendeleaje?" Vema, akasema, "Sasa, asubuhi ni Jumapili." Kasema, "Nyote mnaenda mkutanoni, sivyo?"

165 (Yule mume akasema, "Tutamfanyaje?" Kasema, "Hatuwezi kumpeleka kule namna hiyo!" Kisha kasema, "Vema, sijui la kufanya.") Vema, akasema, "Mama, nakwambia, sisi . . . "

166 "Loo," akasema, "lakini, kipenzi, nisingweza kukaa nje ya kanisa. Hakika kuna kanisa *fulani-fulani* karibu na hapa." "Loo," a . . . akasema . . . Kasema, "Niliona moja kule pembeni, nitaenda tu kule."

(Naye akasema, "Loo, vema, hatuna budi kufanya hivyo.")

167 Kwa hiyo walipoingia, walimwacha aingie kwanza, (Mnaona?) walimwonea aibu. Huyu hapa anavuka barabara na maskini sketi hiyo, mwajua, na Biblia yake chini ya mkono wake. Vema, ndugu, huenda jina lake halikuandikwa kwenye *Nani ndiye Nani,* bali ninawazia jina lake lilikuwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo. Hilo lilikuwa ndilo jambo muhimu.

168 Wakati alipoingia kanisani aliketi chini huko nyuma, akajitwalia kiti, mwajua, na kuifungua Biblia naye akaanza kusoma. Basi kila mtu akaanza kuangalia huku na huku, walidhani namna fulani ya kitu cha kale kilianguka kutoka mahali fulani. Wakiangalia kote namna hiyo, "Loo, jamani!" Huku wamevaa nguo zao zote nzuri, mwajua, Laodikia halisi, na nguo zao nzuri na kadhalika. Waliangalia nyuma wakamwona maskini mama huyu ameketi pale, akiwa na tabasamu kubwa usoni mwake, mwajua, akiisoma Biblia. Naam.

169 Ndipo mchungaji, baada ya kitambo kidogo, baada ya kumalizia mambo hayo mengine yote, hatimaye, alikuwa na hotuba ya karibu dakika kumi na tano. Kwa hiyo akasimama na kusema, "Bwana ni mwema."

170 Huyo mama akasema, "Mungu asifiwe! Hiyo ni kweli! Haleluya!" Basi kila mtu akanyosha shingo yao kama bata, wakiangalia pande zote, "Alikuwa ni nani?"

171 Halafu baada ya kitambo kidogo, akasema, "Uhum! Uhum! Uhum!" Akasema, "Wakristo katika kila wakati wanapaswa

kuwa mashujaa, Wakristo wakuu, wazuri," ama kitu kama hicho.

172 Akasema, "Mungu asifiwe! Hiyo ni kweli!" Na wote wakaangalia kote.

173 Naye, "Uhum!" akaangalia kwenye halmashauri yake ya mashemasi.

174 Ndipo halmashauri ya mashemasi ikapata fununu. Wakaenda kule nyuma wakamshika maskini mwanamke yule mkono wakamtoa nje mlangoni, wakasema, "Unamkatiza mchungaji."

175 Mmekufa wala hamjui! Naam. Loo, hayo madirisha yenu ya rangi yatawafaidi nini? Ni nini benchi zenu zilizopambwa? Na ni nini kusanyiko lenu kubwa? Linaelekea moja kwa moja kuzimuni, kama martini kwenye kasha lake. Kwa maana usipokuwa na Roho wa Mungu, umepotea! Msipozaliwa mara ya pili hamwezi kuuona Ufalme wa Mungu.

176 Hilo ni chungu. Ni kama vile nilivyokuwa nikinywa mafuta ya mbarika, nilisema, "Mama, hata siwezi kuyavumilia."

177 Akasema, "Yasipokuchefua, hayakufai kitu." Kwa hiyo nadhani hivyo ni kama Hili, pia.

178 Loo, laiti ungalizungumza nao! Loo, mijengo mikubwa, mizuri, na kadhalika. Loo, wao—wao—wao . . . Unaenda kanisani mwao, ikitokea useme . . . Uende kanisani mwao na kusema, "Vema, nawaambia, ninyi ni wa Kipentekoste?"

"Loo, naam. Uh-huh. Hakika, sisi ni wa Kipentekoste."

"Mnaamini katika kuzaliwa mara ya pili?"

"Naam."

"Vema, ninataka kuwaonyesha jambo fulani . . . "

179 "Loo, angalia jengo hili! Unajua ni kiasi gani jengo . . . jengo hili limegharimu pesa ngapi? Hilo limegharimu dola robo tatu milioni kulijenga hili. Mwajua, hatukuwa nacho hivyo. Tu—tulikuwa hapa chini kichochoroni." Um-hum, na ukiangalia kote, utaona vitu hivi vyote vikuu walivyo navyo. Naam, bwana. Na ndipo wanasema, "Loo, tuna—tunavyo vitu hivi vyote vikubwa!" Bali hawana mzigo kwa nafsi zilizopotea! Daima wanataka kukuonyesha wana mijengo mingapi. "Hebu angalia taarifa yetu ya shule ya Jumapili, jinsi ilivyo kubwa!" Hiyo ina faida gani iwapo hawana Roho Mtakatifu? "Tajiri, wamejitajirisha, hawana haja ya kitu."

180 Hivyo ndivyo alivyosema, "Mnawazia hayo, bali hamjui ninyi ni maskini, wanyonge, wenye mashaka, vipofu, uchi. Wala hamjui!" Mnaona? Jambo ndilo hilo.

181 Loo, hakika, wao wanasema, "Mnajua nini? Tulikuwa . . . Lile kanisa dogo tulilokuwa tukitumia liko kwenye ile sehemu ya nyuma, hili ni lile kubwa sasa!" Nami nawaambia, hawana

mzigo kwa ajili ya nafsi, bali hawana budi kuona kwamba mambo haya yote yanashughulikiwa. Misaada ya kina mama, na mambo haya mengine yote, yote hayana budi kushughulikiwa, bali hakuna mzigo kwa ajili ya nafsi zilizopotea. Loo, jamani, kile—kile kanisa hili limefikia!

182 Hawakuwa na mzigo kwa ajili ya nafsi, bali walilemewa na mali. Hiyo ni kweli. Walikuwa na mzigo mwingine. Walikuwa na mzigo kwa ajili ya mali yao bali sio mzigo kwa ajili ya nafsi zilizopotea. Maandiko yalisema, "Hawakujua kwamba walikuwa wanyonge," (Loo!) "wenye mashaka, vipofu."

183 Wanafikiri ya kwamba wangeweza kuchukua pesa na kuongoa ulimwengu. "Loo, kama tungeanzisha tu mradi, ambapo tungepata hela nyingi sana hapa, ninaamini tungeweza kuongoa ulimwengu. Kama baadhi ya matajiri kanisani mwetu, Ndugu Branham, kama tungewafanya tu wajitolee kabisa, basi ninaamini tungeanzisha shirika ambalo linge—ambalo lingezunguka na—na kuongoa ulimwengu. Tungechukua ndege na kusambaza vitabu kote Afrika, na mambo kama hayo. Laiti tungalikuwa na pesa!"

184 Ndugu, ulimwengu hautaongolewa na pesa. Ulimwengu utaongolewa na Roho Mtakatifu; kuhubiri kwa nguvu kwa Roho Mtakatifu na Msalaba ndicho kitu pekee kitakachouongoa ulimwengu. Mpango wa Mungu sio pesa. Ni Roho Mtakatifu, huo ndio mpango wa Mungu kwa ajili ya Wakati wa Kanisa la Laodikia ama wakati mwingine wowote wa kanisa. Naam, bwana.

185 Wanamtaka Roho Mtakatifu. Loo, wanasema, "Sisi... tuna dhahabu." Ilikuwa ni dhahabu, kweli, bali sio inayofaa. Walikuwa na dhahabu nyingi bali si zinazofaa. Sasa, kwa hiyo waliamriwa na Yesu, "Ninajua ninyi ni matajiri, na mna dhahabu, wala hamna haja ya kitu," bali:

> *Nakupa shauri* uje *ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto,...*

186 Dhahabu ya aina nyingine, naam, dhahabu iliyosafishwa katika tanuru ya moto, iliyopitia kwenye moto wa mauti, iliyopitia Kalvari, ikatoka.

187 Dhahabu nyingi uliyo nayo itaharibika, itaoza, itaingia kutu. Kama mnaweza kuandika hili, Yakobo... Yakobo Mtakatifu 5:1 hadi 4, nanyi mtapata kile kilicho, ilisema, "Nendeni basi, enyi matajiri, sasa kwenye kule kuja kwa Bwana, lieni mkapige yowe kwa kuwa mashaka yenu yamewajilia, dhahabu yenu imeoza ndani yenu." Mnaona, hiyo ni aina ya dhahabu inayoingia kutu.

188 Bali dhahabu ambayo Yesu hutoa ni Roho Mtakatifu, yale Mafuta ya dhahabu ya Roho Mtakatifu, yanamwagwa moyoni mwako. Na—na, loo, jamani, "Nakushauri, uje ununue kwangu dhahabu, ikiwa unataka kuwa tajiri." Loo, naam.

189 Pia, walikuwa "vipofu." Sasa, ni vibaya kuwa hivyo. Sidhani Wakristo hawa walikuwa vipofu sana kadiri "wasingeweza kuona mbali." Ninaamini wasingeweza kuona mbali. Kitu pekee wangaliweza kuangalia kilikuwa ni mijengo yao mikubwa. Kitu pekee wangaliweza kuangalia kilikuwa ni kusanyiko lao kubwa. Kitu pekee walichoangalia kilikuwa ni kwaya yao iliyopambwa vizuri pamoja na majoho yake yote makubwa na kadhalika. Nafikiri walikuwa tu wasioweza kuona mbali, ilikuwa ni vigumu, kuona kupita pua yao. Sidhani walikuwa vipofu, walikuwa tu wasioweza kuona mbali. Yote wangaliweza kuona yalikuwa ninii yao... "Vema, wajua nini? Sisi ni wa *Hiki-na-hiki*!" Madhehebu yao makubwa, umati wao mkubwa, wafuasi wengi, shule yao ya Jumapili, mijengo yao mizuri.

190 "Bali walihitaji Roho Mtakatifu," Yesu alisema. Walimhitaji Roho Mtakatifu! Kwa hiyo Bwana aliwaambia, "Jicho... Kama ninyi ni... macho ni mabaya sana, nanyi hamwoni mbali sana hata hamwezi kuona chochote ila jengo lenu kubwa hapa na kusanyiko lenu zuri kubwa, na nanii wenu... meya wa mji na wote huja kanisani mwenu, nanyi mna waheshimiwa. Halafu mkanisahau Mimi. Lakini kama ninyi ni vipofu hivyo, na macho yenu yanauma hivyo, nitawauzia dawa ya macho." Naam.

191 Mnaona, ni ajabu kwamba hao madaktari wa uungu hawakuwa na yoyote ya hayo, sivyo? Walikuwa na manukato mengi sana, walikuwa na theolojia nyingi sana. Bali walihitaji dawa ya macho, Roho Mtakatifu wa Mungu, kuyasugua macho yao wapate kukutazamia kuja kwa Bwana, wapate kuiangalia Biblia, wapate kuliangalia Neno. Wanajua jinsi ya kusema "ah-mena" vizuri kabisa. Walikuwa na manukato, walikuwa na mafuta yote. Lakini, "Walihitaji dawa ya macho," Bwana alisema. Kasema, "Mnahitaji dawa kidogo iingie machoni mwenu, nayo itayafungua."

192 Ilikuwa kwamba, wakati nilipokuwa mvulana mdogo... Nimesimulia hili, ninaamini, huenda nililisimulia kanisani. Hili linakuja niani mwangu sasa. Nililelewa katika milima ya Kentucky, kwa sehemu, nasi tuliishi kwenye kibanda cha mbao kilichochakaa. Mama, hapa... Nasi tulikuwa na—tulikuwa na mahali pachakavu kwenye chumba cha juu, na tulikuwa na godoro la—la nyasi kavu. Halafu juu ya godoro hilo la nyasi kavu kulikuwa na la manyoya. Sijui kama mnajua godoro la manyoya ni nini ama hamjui, ama kitanda cha nyasi kavu; kitanda kichakavu, tulikuwa maskini sana. Baba na mama walikuwa na kitanda kidogo kwenye orofa ya chini. Na kwa hiyo tulipanda ngazi ndogo tukapanda juu, naye mama angeweka, wakati—wakati—wakati mwingine, kipande cha chandarua juu ya vitu vya kujifunika na kadhalika, kuzuia... Mwajua, unasimama... unalala pale na kuzihesabu nyota kati ya hizo mbao chakavu zilizowekwa pamoja na nuru ya mwezi, mwajua, na kuna mianya mikubwa kwenye paa namna hiyo.

193 Kwa hiyo wakati theluji ingeshuka ama chochote kile, ama mvua ingetokea, sisi watoto wadogo tungejificha chini ya kipande hiki—hiki cha chandarua, mwajua, kujikinga na hiyo. . . tusije tukalowa maji. Na wakati mwingine upepo kupitia kwenye mianya hiyo, tu—tu—tungeshikwa na baridi na macho yetu yangetoa matongotongo. Mwajua, yanazibwa kabisa na baridi, baridi machoni mwetu. Na kwa hiyo mama angetuita asubuhi, “Shukeni mje.” Ningesema, “Siwezi kuja, mama, maana macho yangu yamejaa matongotongo.” Nina—nina vitu ndani yake, mwajua, baridi kwenye jicho. Tusingeweza kuyafungua, mwajua. Mtoto mdogo amelala pale, nami na Humpy na hao wengine tukijaribu kuyafungua macho yetu wala tusingeweza kufanya hivyo, tumepofushwa.

194 Babu yangu alikuwa mtegaji, aliwatega kuuni, rakuuni. Na huyo alikuwa mponya wote nyumbani kwetu, hayo mafuta ya kuuni. Tulipaka viatu rangi kwa mafuta ya kuuni. Na kama ulikuwa na kifaduro, walinyunyizia terafini kidogo juu yake na kuninii tu, naam, ilikubidi kuyameza, kwa hiyo, kwa ajili ya kifaduro.

195 Basi macho yetu yalipotoa matongotongo sana, mama angechukua kitu hiki. . . “Vema, hebu kidogo, kipenzi.” Alikimbia jikoni akachukua maskini kikombe hiki kikubwa cha mafuta na kukiweka pale, na kuyachemsha sana. Ndipo akaja na kuyasugua macho yetu, mnaona, mpaka yakafanya kazi. Ndipo baada ya kitambo kidogo ikawa ningeweza kuona, nikafungua macho yangu. Kuchukua. . . Mafuta hayo ya kuuni yakayafungua.

196 Nami nawaambia, tumekuwa na upepo mbaya! Mnaona? Kumekuwako na baridi mbaya sana iliyopitia nchini. Wabaptisti walisema, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu, wala hakuna kunena kwa lugha. Hakuna ubatizo katika Jina la Bwana Yesu.” Na, loo, kila namna ya upepo, nao umeyafunga macho mengi sana kwa namna fulani ya baridi ya kiroho. Itahitajika zaidi ya mafuta ya kuuni kuyafungua macho hayo, ndugu. Itahitajika ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu. . .?. . . kuyasugua macho yako ndipo uweze kuona, kukuondolea kutokuona mbali upate kuona Neno la Mungu ni kweli. Hiyo ni kweli. Loo, “Nawashauri kuja mpate dawa ya macho kutoka Kwangu, ile inayoyapaka macho yenu mafuta.” Ili ninyi. . . Ili. . .

197 Madaktari wa theolojia wana ninii yao. . . theolojia yote, na manukato yao na kadhalika, bali ilihitaji zaidi ya hayo. Inahitaji Roho Mtakatifu kutoa ono la kiroho kuona nguvu za Mbinguni zikitenda kazi. Roho Mtakatifu, dawa ya Roho Mtakatifu! Dawa ni mafuta ya moto, tunajua hilo, halafu Roho Mtakatifu ndiye Mafuta ya Mungu.

198 Basi thiolojia yote na manukato, “Loo, ndugu, mpendwa, wewe ni sawa. Hakuna kasoro kwa . . . Kila kitu ni sawa. Vema, tunalo kanisa kubwa kuliko yote mjini.” Manukato hayo hayatafanya kazi! La, bwana! Yatakufanya uone papa *hapa* (kutoona mbali) na kusema, “Naam, tuna kanisa lililo kubwa zaidi ya yote.” Lakini vipi kuhusu Hukumu ijayo wakati Mungu atakapowawajibisha, enyi wafuasi wa kanisa la Laodikia?

199 Sizungumzi sana kwa ajili ya hapa, bali niko kwenye kanda na zinaenda kote ulimwenguni, mnaona, kwa hiyo ninawazungumzia yapata watu milioni kadhaa wakati huu, mnaona.

200 Kwa hiyo jambo ndilo hilo. Laodikia! Vuguvugu! Waliorudi nyuma! Wasioweza kuona mbali! Sijui yote ni nini. Nyumbu! Nyumbu ni chotara, kwanza kabisa yeye hana akili. Ukizungumza naye, yeye anayachomoa hayo masikio makubwa, anasema, “Hoo! Hoo! Hoo! Hoo!” Hana wema wowote. Yeye ni chotara, yeye ni kati ya farasi na punda. Hiyo ndiyo shida sasa, ukiweka Wanikolai na Walaodikia pamoja, unampata punda tena. Tunachohitaji . . . Hiyo ni kweli. Hawajui. Ukiwaambia kuhusu uponyaji wa Kiungu, ubatizo katika Jina la Yesu. Wanasema, “Hoo! Hoo! Mchungaji wangu haninii . . . Hoo! Hoo! Sisi hatuamini hayo kama Wapresbiteri.” Mabaradhuli! Hivyo ni karibu vile ungeliliita . . . ? . . .

201 Ninamchukia nyumbu. Lakini nawaambia, ninapenda farasi mzuri, mpole wa ukoo safi, jamani, unaweza kumfundisha jambo. Unaweza kumfundisha kuinama, na kuingia katika sarakasi, na karibu afanye kama mwanadamu awezavyo, kwa sababu yeye ni . . . anajua jambo fulani. Yeye ni ukoo safi. Nyumbu hajui baba yake alikuwa ni nani au mama yake alikuwa ni nani, wala hawezi kujizaa. Hivyo ndivyo ilivyo na baadhi ya madhehebu haya ya kale, baridi, ya kawaida, kamwe hayawezi kuinuka tena. Mara kanisa linapoingia katika dhehebu, limekufa! Kamwe haliinuki tena. Ni kitu gani? Ni chotara!

202 Martin Luther alikuwa sawa, bali wakati alipounda dhehebu alifanya nini? Methodisti ilikuwa sawa, wakati alipounda dhehebu alifanya nini? Pentekoste ilikuwa sawa, bali wakati mlipounda dhehebu mlifanya nini? Mlilichanganya, mkalizalisha kichotara katika kanisa Katoliki la Wanikolai. Ndivyo hasa mlivyofanya! Mkachukua utaratibu wake wa ubatizo, mkachukua njia zake na matendo yake, nayo Biblia ilisema, “Ninyi ni binti wa kahaba mkuu, malaya. Binti wa makahaba!” Kweli kabisa!

203 Farasi mzuri wa ukoo safi, naam, yeye ni mpole. Loo, ni mzuri, ninampenda. Anaweka kichwa chake juu ya mabega yako, ana upendo, ni mwema. Kwa nini? Anajua baba yake ni nani, anajua babu yake ni nani, anajua baba ya babu

yake alikuwa ni nani. Anaweza kurudi nyuma kabisa, yeye ni ukoo safi.

204 Nami ninapenda kumwona Mkristo halisi wa ukoo safi! Si anayebeba barua yake: yeye ni Methodisti juma lililopita, na Mbaptisti juma hili, na Mpentekoste juma hili, na Mpilgrim Holiness juma lijalo. Hajui baba yake ni nani wala mama yake ni nani. Bali hebu niwaambie, mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu anaweza kukurudisha moja kwa moja hata kwenye Siku ya Pentekoste; anaweza kukwambia yeye ni mpentekoste ukoo safi! Amina! Ninataka kuwa Mpentekoste kutoka juu ya kichwa changu hata kwenye nyayo za miguu yangu. Simaanishi Pentekoste ya kimadhehebu. Ninamaanisha nguvu halisi za Kristo aliyefufuka, Baraka halisi za Kipentekoste.

205 Dawa ya macho, ya kuyafumbua macho yako tuweze kuangalia huko nyuma kabisa na kuona ulikotoka. Unaangalia tu kile kanisa lilicho leo hii; unaangalia nyuma na kuona mahali lilipotoka, kisha unaendelea kusonga mbele kumwelekea Mungu, utayaondokea. Naam, bwana.

206 Vema, niliona jambo lingine, kasema, "Hao ni uchi; uchi wala hawajui." Hakika.

207 Loo, uchi wala hawajui. Sasa, mtu huyo yuko katika hali mbaya sana, kama mtu ni mnyonge, kipofu, mwenye mashaka, uchi. Sasa kama yeye—kama yeye anajua, atajisaidia; bali kama hajui, maskini jamaa huyo amerukwa na akili. Hiyo ni kweli? Whiu! Hilo kidogo lilikuwa ni kali. Amerukwa na akili, hajui vya kutosha kujisaidia.

208 Ukimwona mtu akishuka kuja barabarani, maskini, mwenye mashaka, kipofu, mnyonge, na uchi, nawe useme, "Ndugu, uko uchi." "Loo, kweli? Loo, Loo, ndugu, nisaidie kuingia mahali fulani, nisaidie kupata nguo."

209 Bali ukiwaendea useme, "Aisee, mumempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

210 "Kwani wewe ni nani, mtakatifu anayejibingirisha? Vema, sema, una maana gani? Usinizungumzie namna hiyo, mimi ni Mpresbiteri, mimi ni Mbaptisti, mimi ni wa kutoka *hiki-na-hiki* na *hiki-na-hiki*."

211 Uchi wala hujui! Sasa, mimi kamwe sikusema hilo, Biblia ilisema hilo juu ya wakati huu, "Uchi wala hujui. Njoni mkanunue nguo kutoka Kwangu," Yeye alisema.

. . .*mavazi meupe* . . .

Mavazi meupe ni ya Watakatifu; ndiyo haki ya Watakatifu. Mnaona?. . .

212 Ati uchi? Loo, hakika! Naam, bwana! Loo, mnasema, "Ndugu Branham, sio kanisa letu, ndilo kanisa linalovalia vizuri kuliko yote mjini!" Nisingetilia hilo shaka; baadhi ya mitindo mipya kabisa, vitambaa vilivyokatwa vizuri sana, nguo mpya

kabisa zinazovaliwa na wacheza sinema wa Hollywood, za kizinifu sana zingemvutia kila mwanamume mtaani. Uh-hum. Hakika.

213 Mama mmoja aliniambia, kasema, "Ndugu Branham, unataka kuniambia? Sasa, tunanunua nguo hizi huko madukani na hizo tu ndizo unazoweza kununua."

214 Nikasema, "Wangali wanauza vitambaa na wanatengeneza cherehani. Hamna udhuru mwingi wa kutosha hapo."

215 Biblia ilisema, "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye." Hiyo ni kweli? Vema, basi, kama mwanamke akijivalisha kizinifu na kujianika mbele ya mwanamume, ni nani wa kulaumiwa kwa hiyo? Ni huyo mwanamke, aliisababisha. Hiyo ni kweli kabisa.

216 Sasa, huenda ukawa safi kama yungiyungi kwa mumeo. Huenda ukawa msichana mdogo ambaye hajafanya lolote baya maishani mwako, uwe bikiria utakapoolewa na mumeo. Lakini ukivalia jinsi hiyo na kuwafanya wanaume wakuangalie namna hiyo, yeye amekwisha kuzini *nawe* tayari moyoni mwake. Mwenye dhambi huyo alikuangalia. Kama Mkristo huenda ukawa na nguo zilizoshonwa vizuri kuliko zote mjini, zilizo nzuri sana za manyoya, bali haimpasi Mtakatifu wa Mungu kuvalia namna hiyo.

217 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Loo, naam, usimjie mwana wa Mungu.

218 "Loo, la," wao wanasema. Vema, wao wanasema, "Kanisa letu..." Mmevalia vizuri? Walisema ndivyo. Walikuwa "matajiri, hawakuwa na haja ya kitu." Hakika. Mbona, wao walisema, "Hata mchungaji wetu anatembea amevalia vazi kubwa kuu mno. Kwaya yote inatembea huku imevalia vazi kubwa kuu mno." Ibilisi amebingirishwa ndani yake. Uh-hum. Uh-hum, hiyo ni kweli. Loo! Hmm, hmm! Vema, afadhali nisiseme hilo lingine pia. Kwa hiyo, huenda nikaachilia hilo. Vema.

219 Loo, mambo haya yote makubwa! Kwaya zilizovalia majoho, kwaya za kulipwa, inawabidi kuwalipa wapate kuimba. Hmm. Inawabidi kumlipa mhubiri kiasi fulani la sivyo atapata wengine wanaomlipa vizuri zaidi kidogo. Ataita halmashauri ya wadhamini na kusema, "Sasa, ndugu, mimi—mimi...mmekuwa wema sana kwangu hapa, mnanipa mia *kadhaa* kwa juma," ama kitu kama hicho. "Lakini Kanisa lile jingine la Presbiteri la..." (Liiteni "Pentekoste" ama chochote lilicho.) "huku, wame—wameahidi ya kwamba watanipa *kiasi fulani* zaidi." Loo, jamani!

220 Basi mtakatifu maskini ana nini? Wana nafasi gani? Maskini kanisa dogo lililojazwa na Roho Mtakatifu lina nini, wana nafasi gani? Wasingeweza kumudu chochote kama hicho. Kwa hiyo Bwana huwainulia tu kitu fulani basi, amina, ambacho

amekichagua Mwenyewe, akakijaza na Roho Mtakatifu na kumweka kama msimamizi mkuu juu yake. Anashusha... Yeye alisema, "Nakushauri uje ununue mavazi meupe kutoka kwake." Biblia ilisema, "Mavazi meupe ni matendo ya hak-... ya watakatifu."

221 Sasa, ninaamini sisi...Hebu tufikie kwenye—kwenye kifungu cha 19 sasa. Ninaamini tuko kwenye yapata kifungu cha 20, vizuri sana niwezavyo kuona. Naam, naam, na ninafunga kwenye hili. Sasa, iweni wanyamavu sana sasa na msikilize sasa wakati tukifanya jambo hili. Sikilizeni:

> *Tazama, nasimama mlangoni, nabisha: mtu akiisikia sauti yangu, na kufungua mlango, nitaingia...nami nitakula pamoja naye, naye pamoja nami.*
>
> *Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami* katika *kiti changu cha enzi, kama mimi* nilivyoshinda, *nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi.*
>
> *Yeye* aliye *na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.*

222 Hili ni moja ya matamshi dhahiri sana ambayo nimewahi kuona katika Agano Jipya. Ninawatakeni mwangalie, "Nasimama mlangoni nabisha." Hili kwa jumla linatumika, nukuu kwa ajili ya kuwashawishi wenye dhambi. Hiyo ni kweli? Tunawaambia wenye dhambi, "Yesu yuko mlangoni, anabisha." Lakini hapa Yeye anabisha mlangoni pa *kanisa* kwa kuwa wakati mmoja Yeye alitembea pamoja nao, bali wao (pamoja na dhehebu lao na mambo ya kilimwengu na ubaridi) walikuwa wamemwondosha. Yeye yuko nje ya kanisa.

223 Sasa, kumbukeni, mwanzoni mwa nyakati za kanisa, tunapofunga, Yeye alikuwa akitembea miongoni mwa vinara saba vya taa vya dhahabu (Hiyo ni kweli?), nyakati saba za kanisa. Na hapa mwishoni, tunamwona nje ya kanisa lipi? Lile la Laodikia, kanisa la Laodikia. Nje, walikuwa wamemwo-... wamemweka nje. Mbona, Yeye alikuwa amesimama nje akijaribu kuingia. Ni picha ya kusikitisha jinsi gani! Mwokozi wa ulimwengu, akisimama nje ya kanisa alilonunua kwa Damu Yake Mwenyewe. Aibu kwao!

224 "Nasimama mlangoni na kubisha." Baada ya kusukumwa nje ama kutolewa, kisha kujaribu kurudi ndani, anatambaa na kubisha mlangoni. Hii ndiyo kumbukumbu ya kushtusha sana katika Agano Jipya. Nafikiri hakuna kitu kingaliweza kuwa cha kuhuzunisha sana kuliko hiki, kumwona Mwokozi wa ulimwengu amefukuzwa kanisani Mwake Mwenyewe, wakati wa kanisa la Laodikia. Baada ya kuwaambia yale waliyokuwa wamefanya, utajiri wao na kila kitu, na kile walichokuwa, na jinsi walivyokuwa na uvuguvugu na kadhalika, na wao—wao walikuwa na...wao...Haikumbidi kuwatapika, walikuwa wamemtapika *Yeye*. Na hapa palikuwa na hayo yote, angali

anabisha mlangoni, akijaribu kuingia ndani tena. Kwa nini? Kuwapa Uzima wa Milele. Wale wale waliomwua pale Kalvari, alikuwa akijaribu kuiokoa nafsi yao. Ndiyo picha ya kusikitisha kuliko zote niliyopata kuona maishani mwangu, niliyopata kuwazia.

225 Kuondolewa! Aliondolewa wapi? Sasa, sikilizeni, enyi marafiki. Kama hili si la kushtusha! Pateni picha yake, hebu na izame moyoni mwako. Mwokozi wetu, wakati alipokuwa duniani, Yeye aliondolewa kwenye taifa Lake Mwenyewe. Alikataliwa, aliondolewa. Ulimwengu ulimwondosha na kumsulubisha. Na sasa, kutoka kwenye kanisa Lake Mwenyewe, Yeye ameondolewa. Hatakikani popote, hawana haja Naye. Wana dhehebu, hawakumhitaji. Wana papa, wana haja gani Naye tena? Wana askofu mkuu, mwangalizi mkuu, hawakuwa na haja ya Roho Mtakatifu tena. Hawakumhitaji Huyo tena. Kristo, Roho Mtakatifu, hawakumhitaji. Kwa hiyo wao ni . . .

226 Siamini walisimama tu na kumtupa nje, maana hawakuwa wamemwonea shauku. Hawakuwa wamemwonea shauku, kwa kuwa wangali walikuwa wakimwimbia nyimbo. Mhubiri alikuwa angali anazungumza juu Yake, kwa hiyo hawakuwa wamemwonea shauku. Bali mambo yao wenyewe ya kilimwengu na dhehebu lao, likijipanga, likisema, "Siku za miujiza zimepita wala hakuna kitu kama *hiki* na *kile*."

227 Ninawauliza. Kila uamsho uliowahi kuja (wowote, ninyi wanahistoria), sasa, kote kote kupitia hapa, makanisa haya, kila uamsho uliowahi kuja, ninii . . . daima ulileta nje ya dhehebu. Mtu yeyote aliyepata kuanzisha uamsho, alikuwa nje ya madhehebu. Na kila wakati u—uamsho ulipoanza, walikuwa na ishara na miujiza ya kunena kwa lugha na uponyaji, na kadhalika namna hiyo, yakitukia. Mara huyo mwanzilishi alipokufa, basi waliuundia dhehebu na kufanya shirika kutoka kwake, nalo "likafa" mara moja wala Mungu hakushughulika nalo tena. Hiyo ni kweli kabisa.

228 Naye huyu hapa kwenye wakati wa mwisho wa kanisa, amesimama nje mlangoni, Mungu Mwenyezi. Hilo—hilo linauvunja moyo wangu kuwazia hilo. Bwana wangu akisimama nje mlangoni mwa kanisa Lake Mwenyewe, baada ya kusukumwa nje na mambo ya ulimwengu na ubaridi na dhehebu na kutojali, amesimama nje ya mlango, anabisha, akijaribu kurudi ndani. Nilipowazia hilo, muda mfupi uliopita, niliinama tu mezani pangu nikaanza kulia. Nikawazia . . .

229 Mara nyingi nimewazia, wakati Yesu alipokuwa ameketi nyumbani mwa maskini Mfarisayo yule pale, hakuna mtu aliyemshughulikia, alipokuwa na miguu michafu. Hawakumlaki mlangoni na kuiosha miguu Yake na kumpaka mafuta, kumwondolea samadi na takataka za mahali alipokuwa ametembea; vazi Lake likifagia kote, likaleta maskini harufu

hiyo ya barabarani ambamo farasi na kadhalika walikuwa wamesafiria, na—na kumfanya anuke.

230 Sikuzote wangeosha miguu, hiyo ndiyo iliyokuwa desturi. Naye mtumishi mwosha miguu alikaa mlangoni. Basi mtu alipokuja, wangeosha miguu yake, na kunyosha mkono pale na kuchukua maskini jozi moja ya ndara zilizomtosha, na kumvalisha. Nao wakamtia mafuta kichwa chake na ninii yake. . .na kumfanya anukie vizuri, na kule kuchomwa na miali ya jua shingoni mwake, wakachanua nywele zake. Akaingia ndani.

231 Na kukaribishwa kwa mgeni, sasa hivi ndivyo wao. . .Hebu simama hapa dakika moja, Pat, ninataka kuwaonyesha jambo fulani. Hivi ndivyo walivyofanya, wangemkaribisha hivi. Sasa, ninaamini. . .La, kama hapa, ninaamini ni kitu kama hiki hapa, kukaribisha namna *hii,* mnaona, na kukumbatiana. Naye alikuwa amekaribishwa.

232 Bali Yesu alipokuja kwenye karamu hii, kama tu vile alivyokuja kwenye karamu ya Kipentekoste hapa, mtu fulani alikuwa amemkosa. Walivutiwa sana na mambo yao, maaskofu na kadhalika walikuwa pale. Yesu alialikwa bali hakuna mtu aliyeitawadha miguu Yake. Naye huyo hapo alikuwa amaketi pembeni, ilikuwa vigumu kwao kujua alikuwa pale, huku miguu Yake inanuka, uchafu mwilini Mwake mwote, amejaa mavumbi.

233 Halafu kuna maskini kahaba mmoja huko chini mtaani aliyekuja pale, alikuwa tu na fedha kidogo kwenye pochi lake. Basi akaangalia huko akamwona Yesu ameketi pale mwenye miguu michafu. Iliuvunja moyo wake. Akasema, "Huyo ndiye yule mtu aliyemsamehe yule mwanamke dhambi zake. Huyo ndiye yule mtu ambaye nimesikia kwamba ameponya watu. Kwa nini wasimjali?"

234 Kwa sababu maaskofu na hao wote walikuwa huko, walimwondosha nje. Huyo pale . . . Walimwalika aje.

235 Hivyo ndivyo tunavyofanya. Tunamwalika kuja kwenye mikutano yetu, bali tunapokuja tunamwonea aibu. "Loo, nisingekaa na kusema 'Bwana asifiwe.' Loo, la, wale pale akina Jones wameketi, watafikiri mimi ni mtakatifu anayejibingirisha." Ewe mnafiki! Hiyo ni kweli. "Nahofu ningenena kwa lugha nao wangeniita 'mwanalugha.'" Wewe ni mwenye mashaka mno!

236 Sasa, kumbukeni, hili linaingia, mnaona. Wewe ni mwenye mashaka, mnyonge, maskini, uchi, na kipofu, wala hujui.

237 Yesu ameketi pale na miguu michafu. Naye kahaba wa mtaani, ningeweza kumwona akishuka, hebu—hebu tuzungumze. . .tumchukue kwa dakika moja. Ninaweza kumwona akishuka kwenda dukani, naye anasema, "Mimi . . ." Ndipo machozi yakaanza kutiririka usoni mwake, naye akasema, "Si—siwezi kulifanya. Kama—kama—kama nikipeleka

kitu hiki pale, Yeye atajua mahali nilipopata pesa hizi. Anajua jinsi nilivyozipata, bali ndizo kitu pekee nilicho nacho."

238 Hayo tu ndiyo anayotaka. Hayo tu ndiyo anayotaka. Mnaona? Yeye hajali. Njoo tu, "Sina cha mkononi."

239 Kwa hiyo alichukua manukato na kuyaleta. Naye akaenda pale akawazia, "Loo, laiti ningalimwona!" Ndipo akaingia kisiri na akaingia mlangoni mahali fulani.

240 Na, la, hawakuwa wamemkaribisha. Kwa hiyo akachukua kibweta hicho na kukivunja na kuyaweka juu ya ninii yake. . . juu ya miguu Yake, na akaanza kuiosha miguu Yake. Ndipo akaanza kulia, "Loo, hapana shaka ni Yeye. Huyo Ndiye ambaye sikuzote nimesoma habari zake katika Biblia. Ninajua atatambua jambo hilo." Na muda si muda wajua. . .Ni maji mazuri jinsi gani kwa miguu Yake, machozi ya toba yakitiririka miguuni Mwake. Hakuwa na kitambaa cha kupangusia miguu Yake, kwa hiyo akanyosha mkono na kushika nywele zake. Mawimbi yake mazuri ya nywele yakavurugika, machozi yakitiririka usoni mwake namna hiyo. Akaiosha miguu Yake, na mara kwa mara [Ndugu Branham anatoa sauti ya busu—Mh.] angeibusu miguu Yake, akaiosha miguu Yake namna hiyo.

241 Yesu akiwa na miguu michafu, wala hakuna mtu anayeijali hiyo. Na leo hii ana jina baya kama mtakatifu anayejibingirisha, ama kitu kama hicho, wala watu hawana ujasiri wa kumtetea.

> Msalaba huu uliowekwa wakfu nitaubeba,
> Mpaka mauti itakaponiweka huru,
> Nitaambatana na wachache wa Bwana waliodharauliwa,
> Nimeanza pamoja na Yesu, Ee Bwana, nifanikishe. (Nifanikishe, Bwana, hata ikigharimu nini.)

242 Ninayo, kama Yakobo, mto wa kulalia, jiwe. Inaleta tofauti gani? Kile Yeye alichonifanyia!

243 Na maskini kahaba huyu pale, akilia, akiomboleza. Na muda si muda mwajua, huyu hapa Simoni amesimama, yule jamaa mkubwa aliyemfanya ashuke aje, kasema, "Uhm, uhm, uhm, uhm! Hiyo inaonyesha kama Yeye ni nabii ama sivyo, angejua yeye alikuwa ni mwanamke wa aina gani." Mnafiki huyo!

244 Basi baada ya kumaliza. . .Na Yesu kamwe hakuusogeza mguu Wake, Yeye aliketi tu na kumwangalia na kumtazama. Loo, ninapenda jambo hilo. Si yale mambo makubwa tunayofanya, wakati mwingine ni yale mambo madogo tunayoyaacha bila kuyafanya. Yeye alimwangalia, akamwangalia tu ameketi pale. Hakuna mtu aliyekuwa akimjali; hatimaye, yeye pale ndani akilia na kuiosha miguu Yake, kwa namna fulani akalishughulikia, akawavutia watu. Na Yeye akamwangalia tu, kamwe hakusema neno.

245 Maskini Simoni akisimama pale nyuma, kasema, “Uhm! Mnaona kama Yeye ni nabii ama siye, sivyo? Niliwaambia! Niliwaambia! Angalikuwa ni nabii, angejua mwanamke huyo alikuwa ni nani. Mnaona, tulikuwa ndio kanisa kuu hapa, mnaona, tunajua, hivyo. Tunajua Yeye si nabii, angejua hilo.”

246 Akiisha . . . Akiisha kumaliza, hayo machozi ya toba yakitiririka usoni mwake, yaliiosha miguu ya Yesu. Yeye . . . ninaamini alijisikia kidogo ameburudika.

247 Ee Mungu, laiti ningalikuwa pale! Ningaliiosha tena. Naam, bwana.

248 Jamani, mwanamke si angekuwa na wakati mgumu akiipangusa miguu hiyo kwa nywele zake siku hizi? Ingemlazimu kusimama kwa kichwa chake kufanya hivyo, kupata nywele za kutosha kuipangusa. Naam, bwana, wanazinyoa zote.

249 Lakini hapo, miguu ya Yesu, hakuna mtu anayejali . . . (kukosoa), ameketi ameaibika, harufu hiyo miguuni Mwake. Huyo mwanamke alimwosha. Baada ya Yeye—baada ya Yeye kumaliza, Yeye aliinama akamwangalia huyo mwanamke kama kusema, “Vema.”

250 Akaangalia huku, kasema, “Simoni, ninalo jambo la kukwambia. Ulinialika hapa, wala hukunilaki mlangoni. Hukunipa maji yoyote ya kuoshea miguu Yangu. Hukunipaka mafuta kichwa Changu nilipoingia, kuniondolea mchomo wa jua. Hukunipa busu lolote la kunikaribisha nilipoingia. Bali maskini mwanamke huyu,” (Loo, jamani.) “huyu mtu wa nje, kahaba mtaani, hakuwa na maji ya kuitawadha miguu Yangu ndipo akaitawadha kwa machozi yake. Hakuwa na kitu cha kuipangusia, kwa hiyo akachukua nywele zake, akaipangusa. Ameendelea kuibusu miguu Yangu. Sasa nataka kukwambia: dhambi zake, ambazo zilikuwa nyingi, zimesamehewa.” Hiyo ni kweli, kamwe hakusema lolote kuhusu zake. “Dhambi zako, ambazo ni nyingi, zimesamehewa.”

251 Na leo hii wakati Yesu, akisimama nje ya mlango wa madhehebu ya Kipentekoste, madhehebu ya Baptisti, madhehebu ya Kimethodisti, akijaribu kurudi ndani pamoja na pentekoste tena, nao watu wanampita. Baada ya wewe . . . mambo yenu ya ulimwengu na kadhalika yamemsukuma nje ya kanisa, Yeye amesimama, akijaribu, akilia apate kurudi ndani tena. Na, loo, ndilo jambo la kuhuzunisha kuliko yote nililopata kuona maishani mwangu. Hawakuwa na haja Naye! Yeye, nje, akibisha, akijaribu kuingia ndani. Hilo ndilo jambo lile lile analojaribu kufanya. Kwa nini? Kwa nini? Yeye alikuwa nje.

252 Kamwe hawakumtupa nje. Wangali waliimba juu Yake, wakahubiri habari Zake, bali kamwe hawakuwa wamemwonea shauku mbele zao. Hiyo ni kweli. Walikuwa wakiendelea moja kwa moja. Kwa nini? Walikuwa hawaoni mbali. Walikuwa wakiangalia jengo lao kubwa. Walikuwa matajiri. Walikuwa

wakiangalia hilo dhehebu kuu ambalo walikuwa wafuasi wake, wakijaribu kulijenga, wakiwaingiza wafuasi wengi zaidi, wala hawakumwonea shauku. La, la. Hawakuwa na shauku ya kunena kwa lugha. Hawakuzionea shauku zile jumbe kuu, zenye nguvu za Mungu Yule ambaye hukata hata kwenye moyo na kuutahiri moyo, hurarulia mbali mambo ya ulimwengu na kukumenya kama kipande cha mahindi. Loo, wao . . .

253 Kama ulihubiri hivyo kanisani mwao, wangekutoa nje. Na hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyohubiri. Yesu alisema, "Enyi kizazi cha nyoka! Ninyi—ninyi nyoka nyasini!" Naye Yohana akahubiri hivyo, pia, na watu mashuhuri waliopakwa mafuta, daima waliwachana ngozi. Hiyo ni kweli.

254 Lakini hawakumwonea shauku, maana hawakuwa na Huyo. Mnaona? Kwa hiyo walikuwa na maskini kitu kidogo cha kimaua kikiwapiga-piga mgongoni, na kusema, "Wewe jiunge tu, andika jina lako papa hapa, na—nasi tutakuchukua kwa uanachama wako. Nawe uende ukachukue karatasi yako kutoka kwa kanisa hilo lingine nasi tutakupokea, na—na kadhalika. Sasa, nadhiri yako itakuwa ni ngapi kwa kila mwaka?" Mnaona, jambo ndilo hilo, "Tajiri, hawana haja ya kitu." Loo! Bali mna haja na kitu kilicho kikubwa sana wala hamjakipata, Yesu akisimama nje akijaribu kuingia kwa pentekoste.

255 Unafikiri ni kitu gani kingetukia usiku wa leo katika kanisa la Kimethodisti kama Roho Mtakatifu angeshuka juu ya kanisa nao waanze kupiga makelele, wakiruka-ruka, wakinena kwa lugha na kufanya kama walevi . . . kundi la walevi? Mbona, lile—lile Kongamano lingeliondosha kanisa hilo la Methodisti kutoka kwenye Kongamano. Mnajua hilo. Ingekuwaje katika kanisa la Baptisti kama lilitukia? Jambo lile lile. Wapentekoste? Mbona, kuna wengi wao, jambo lilo hilo lilitukia. Hakika. Naam, bwana, wasingevumilia upuuzi kama huo. Wangesema, "Mbona, hata waliyaharibu mazulia yetu mapya." Uh-hum, hakika. Jamani! Jamani! Ni kundi lenye mashaka jinsi gani. Hiyo ni kweli.

256 Vema, sawa, Yeye alikuwa nao wakati mmoja, alitembea pamoja nao katikati ya vinara vya taa saba vya dhahabu. Basi hili hapa jibu: madhehebu na mambo yao ya kilimwengu, maaskofu wao, makadinali, na mambo yao yote ya kilimwengu, yalikuwa yamemwondosha na kamwe hawakumwonea shauku. Nalo kanisa . . .

257 Sasa, tutafanya nini kumrudisha ndani? Ikiwa Yeye yuko nje ya kanisa la Kipentekoste sasa, tutafanya nini kumrudisha ndani? Je, itahitaji kura ya kauli moja ya watu kumrudisha? Itahitaji kuchaguliwa kwa papa mpya, kadinali mpya? Ama labda itahitaji—ita—itahitaji kuinua dhehebu jipya. Hilo halitamleta kamwe! Hilo halitafanikiwa kamwe. Dhehebu jipya halitaweza, nanii mpya—ka—ka—ka—ka—kadinali mpya hataweza, mchungaji mpya hataweza, mwinjilisti anayelipwa

vizuri hataweza. Hakuna kitu ulimwenguni kinachoweza kufanywa ila wewe mwenyewe. Tunaingiaje ndani Yake? Si kwa kura. La, bwana. Hatumpigii kura Yesu arudi ndani, maana hatarudi.

258 Hili—hili hapa, “Mtu akiisikia Sauti Yangu na kufungua mlango.” Sasa, tunajua mlango ni nini basi. “Mtu akifungua mlango, akiisikia Sauti Yangu.”

259 Si—si “Kama kanisa lolote . . . Kama dhehebu lolote . . . ” La, bwana. Yeye hajishughulishi nayo, yamekufa na kuisha kwanza. Yeye anayachukia, sikuzote aliyachukia. Alisema aliyachukia! Naye anayachukia bado usiku wa leo!

260 “Lakini mtu yeyote,” Mmethodisti yeyote, Mbaptisti yeyote, Mpresbiteri yeyote, ama Mkatoliki yeyote, mtu yeyote wa Church of God, Mnazarayo, Mpentekoste. “Mtu yeyote atakayeisikia Sauti Yangu na kufungua mlango, nitaingia na kula pamoja naye naye pamoja Nami.” Huo ndio ujumbe kwa kanisa la Kipentekoste. Si kujaribu kulifufua dhehebu la Kipentekoste, bali kuzifufua Baraka za Kipentekoste katika moyo wa mtu binafsi. Hiyo ndiyo njia pekee. “Nami nitakula pamoja naye, naye, Mimi.”

261 Ni nini mjumbe wa kanisa . . . ujumbe kwa kanisa unatufundisha nini basi, kufundisha—kutufundisha? Sio kukua katika Roho. La, bwana. Kudhoofika kwa Roho, tuna kudhoofika wakati wote. Njia . . . Wa—wale wajumbe kwa kanisa na ujumbe kwa kila wakati wa kanisa ulihukumu umadhehebu. Kila ujumbe kwa kanisa, kanisa lilikuwa daima linadhoofika wala halingeusikia. U—ujumbe kwa kanisa ulikuwa ni kuyapuuzia madhehebu. Nayo yalisababisha Wakristo chotara, wanavyojiita, hiyo ni kweli, wasiojua lolote kumhusu Mungu wala Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli tu kama ninavyosimama hapa jukwaani usiku wa leo. Hao wafuasi wazuri vuguvugu, wapate tu kutapikwa kutoka kinywani Mwake.

262 Paulo alionya, Mataifa yalikuwa ni tawi. Sasa, ninawataka baadhi yenu, mkiweza, mfungue Warumi, mlango wa 11, kifungu cha 15 hadi kifungu cha 27, kusudi tu mwiandike, ninyi nyote. Halafu basi, kwa kuwa tumechelewa, nitawanukulia hili sasa kabla tu ya kuondoka, kwa maana ni ninii . . . Sasa, Warumi, kama mkitaka kuiandika, 11:15 hadi ishirini . . . hadi 27. Paulo aliwaambia, aliwaambia, akinena na Mataifa pale, wale Warumi, yeye alisema, “Ikiwa Mungu . . . ” Sasa, sikilizeni tunapomalizia nyakati za kanisa! Paulo alisema, “Ikiwa . . . Mungu hakuuacha mzeituni asili, bali aliukata kwa sababu ya kutokuamini.”

263 Hiyo ni kweli? Ni kwa nini walikatwa? Kwa sababu waliikataa pentekoste. Hiyo ni kweli? Kwenye Siku ya Pentekoste walimdhihaki na kumkufuru Roho Mtakatifu.

264 Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema. . . Waliita—walimwita, "Beelizebuli," kasema "Yeye alikuwa ni ibilisi," na "Yeye ni mpiga ramli," chochote zaidi.

265 Yeye alisema, "Ninawasamehe hilo, bali wakati Roho Mtakatifu atakapokuja msiongee dhidi Yake; maana mkiongea dhidi Yake, hamtasamehewa."

266 Pia kumbukeni wakati Yesu alipowaagiza wanafunzi Wake, "Msiende kwa mataifa." Hiyo ni kweli? "Bali mwende kwa kondoo waliopotea wa Israeli."

267 Walijihukumuje? Kwa kumkufuru Roho Mtakatifu, kumwita Roho wa Mungu "kitu kichafu." Wakamdhihaki wakati walipokuwa wakicheza katika Roho, na kadhalika, kwenye Siku ya Pentekoste. Mji uo huo, waliufanyia mzaha, Tito aliwaulia mle ndani nayo damu yao ikatiririka kutoka langoni. Waliwala watoto wao wenyewe, na kila kitu, katika karne iyo hiyo. Na hiyo ni kweli. Moja ya mataifa yaliyo makuu sana ulimwenguni likawa lililo duni sana, na kutawanyika kwenye ki-. . . pepo nne za dunia. Kwa sababu gani? Kutokuamini! Na hicho kilikuwa ndicho kisiki asilia, mti asili, Israeli.

268 Hivi Paulo hasemi pale? Ni nani aliye na Maandiko papo hapo? Umeipata, Pat? Simama usome kutoka kifungu cha 15 hadi 27.

> [Ndugu Pat anasoma: *Kwa maana ikiwa kutupwa kwao kumeleta upatanisho kwa ulimwengu, je, kukataliwa kwao—kwao kutakuwa nini kama si uhai baada ya kufa?*—Mh.]
>
> [*Tena malimbuko yakiwa matakatifu, kadhalika na donge lote: na shina likiwa takatifu, matawi nayo kadhalika.*]
>
> [*Lakini iwapo matawi mengine yamekatwa, na wewe mzeituni mwitu ulipandikizwa kati yao, ukawa mshirika wa shina la mzeituni na unono wake;*]
>
> [*Usijisifu* mwenyewe *juu ya matawi yale; au ikiwa wajisifu, si wewe ulichukuaye shina, bali ni shina likuchukualo wewe.*]
>
> [*Basi utasema, Matawi yale yalikatwa kusudi, ili nipandikizwe mimi.*]
>
> [*Vema. Yalikatwa kwa kutokuamini kwao, . . .*—Mh.]

Sikilizeni, "Kutokuamini!" Vema, endelea.

> [. . . *na wewe wasimama kwa imani yako. Usijivune, bali uogope:*—Mh.]
>
> [*Kwa maana Mungu hakuyaacha matawi ya asili, wala hatakuachia wewe.*]
>
> [*Tazama, basi, wema na ukali wa Mungu: kwa wale walioanguka, ukali; bali kwako wewe, wema, ukikaa*

katika wema wake: kama sivyo, wewe nawe utakatiliwa mbali.]

[*Na hao pia, wasipokaa katika kutokuamini kwao, watapandikizwa: kwa kuwa Mungu aweza kuwapandikiza tena.*]

[*Kwa maana ikiwa wewe ulikatwa ukatolewa katika mzeituni, ulio mzeituni mwitu kwa asili yake, kisha ukapandikizwa, kinyume cha asili, katika mzeituni ulio mwema: si zaidi sana wale walio wa asili kuweza kupandikizwa katika mzeituni wao wenyewe?*] Hmm.

[*Kwa maana, ndugu zangu, sipendi msijue siri hii, ili msijione kuwa wenye akili; ya kwamba kwa sehemu ugumu umewapata Israeli mpaka utimilifu wa Mataifa uwasili.*]

[*Hivyo Israeli wote wataokoka: kama ilivyoandikwa, Mwokozi atakuja kutoka Sayuni, atamtenga Yakobo na maasi yake:*]

[*Na hili ndilo agano langu nao, nitakapowaondolea dhambi zao.*]

269 Mnalipata? Paulo alisema, "Ikiwa Israeli walikuja na kuona ishara hapa za Roho Mtakatifu, nao wakakatiliwa mbali . . ." Kumbukeni, kwa sababu waliukataa ujumbe wa Paulo (ubatizo katika Jina la Yesu, toba na ubatizo katika Jina la Yesu, ishara na maajabu yakimfuata mwaminio) nao wakaukataa. Nao wakasema:

. . . lo, tutawaendea Mataifa.

270 Hiyo ni kweli? Hebu tuone, ninaamini ilikuwa kwenye . . . mahali walipoitwa Wakristo kwa mara ya kwanza, ilikuwa huko Efeso, Vema, Antiokia.

271 Sasa—sasa, kama—kama mti wa kwanza ulikuwa ni mtakatifu, matawi yake matakatifu, ule mti wa asili, na kwa sababu hawakuuamini Ujumbe wa Kipentekoste ambao Paulo alikuwa akihubiri (Hiyo ni kweli?), Mungu aliwakatilia mbali na kuchukua mzeituni mwitu (ambao ulikuwa ni Mataifa, sisi) na kutupandikiza tupate kuishi kwa ta- . . . nguvu za mti huo.

272 Sasa, ni zaidi sana vipi katika siku hii wakati tunaukataa Ujumbe wa Kipentekoste ambao umeshuka kupitia nyakati za kanisa, ni zaidi sana vipi Mungu anavyoweza kuutoa huo mti mwitu kwake, kwa vyovyote vile, na kuuacha huo mwingine uingie? Kwa sababu ataukataa, kwa sababu ya kutokuamini. Sasa ambatanisha hilo na ujumbe asubuhi ya leo. Mnajua mahali tunaposimama sasa, sivyo? Tuko kwenye wakati wa mwisho kwa ajili ya kuchukuliwa kwa Kanisa la Wamataifa, Unyakuo Wake; na kutolewa kwa Roho Mtakatifu kuja juu ya Wayahudi, na Yesu kujitambulisha Mwenyewe, kuwatia muhuri wale mia moja na

arobaini na nne elfu. Haya basi. Kuurudisha ule mti wa asili (kuurudisha kwenye Baraka) katika Israeli tena.

273 Yesu hatasimama nje ya mlango wako na kubisha wakati wote. Kuna wakati ambapo atapata ya kutosha na kuondoka, ndipo wewe nawe utabisha bali kamwe hutampata. Njoo wakati ungalipo. Njoo wakati kunabishwa. Usipatane na chochote pungufu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu kama walivyompokea huko Pentekoste, pamoja na ubatizo ule ule wa maji, mambo yale yale waliyofanya kule. Usiache chochote kiweke kitu chochote moyoni mwako pungufu ya huo.

274 Sasa, kwenu ninyi rafiki zangu Wakatoliki, hebu niwaambie jambo fulani, mnamwamini bikira Mariamu. Bikira Mariamu, akiwa ni mama wa Yesu Kristo, ilimbidi kwenda hadi Pentekoste na kujazwa na Roho Mtakatifu, naye akatenda kama mlevi. Alikuwa miongoni mwa hao mia na ishirini, waliokuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, akinena kwa lugha na kufanya kama mwanamke mlevi huko nje, chini ya Roho wa Mungu. Na kama ilimbidi bikira Mariamu kufanya hivyo kusudi aingie Utukufuni, wewe utaingiaje Kule, chochote pungufu ya huo? Wazia hilo. Hiyo ni kweli.

275 Wabaptisti . . . Huyo mhubiri wa Kibaptisti hapa nyuma anataka kuwa na uhakika limesemwa kwa Wabaptisti pia. Huo ni kwa mtu yeyote, sijali yeye ni nani.

276 Kwa hiyo kujiunga tu na kanisa na kukariri kanuni ya imani, na kwenda kanisani kila Jumapili asubuhi, hakutakusaidia hata chembe moja. Unamdhihaki tu Mungu. Ama uwe Mkristo halisi au usiwe kitu chochote kamwe. Uwe moto ama baridi. Ama uwe nje . . . Kwa sababu huwezi kuwa . . . Kamwe hujapata kumwona ndege mweusi mweupe, kamwe hukuona mlevi asiye mlevi, kamwe hukumwona mwenye dhambi-mtakatifu. La, huwaoni, hawawawafanyi. Ama umejazwa na Roho Mtakatifu na Mungu anaishi ndani yako, ama hujajazwa kabisa. U—umejazwa au hujajazwa.

277 Kwa hiyo basi huna budi—huna budi kukumbuka ya kwamba Yesu anasimama mlangoni pako, pia kumbuka ahadi ya Mungu hapa ya kwamba atafanya hivyo katika siku hizi. Kwa sababu gani? Kukataa. Ni kitu gani kilisababisha kukatiliwa mbali kwa Israeli, ule mti asilia? Kwa sababu waliukataa Ujumbe wa Kipentekoste wa Paulo. Na je, mnaamini huu ndio wakati wa mwisho wa kanisa? Biblia ilisema hivyo! Nayo inasema itakuwaje kwao? Watakatiliwa mbali kwa sababu ya kuukataa Ujumbe wa Kipentekoste, ndipo Mungu atarudi tena kwa Wayahudi.

278 Ndipo Israeli wote basi wataokolewa, maana atawachukua kama taifa, sio kama mtu binafsi. Bali kwako wewe na mimi ni mtu binafsi, kwa sababu Yeye huja kwa Wayahudi . . . Matendo, katika Kitabu cha Matendo, Yeye alikuja kwa Mataifa

kuwachukua "watu kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lake," Bibi-arusi Wake. "Watu," mmoja hapa, mmoja pale, mmoja huku, Naye anatushughulikia kama watu binafsi, na bila kujali jamii, kanuni ya imani, wala rangi. Yeye hutushughulikia kama watu binafsi, ndio shada Lake atakaloliweka kwenye madhabahu Yake. Lakini kama Wayahudi, Yeye daima aliwashughulikia Israeli kama taifa, hao ni taifa la watu, taifa Lake.

279 Nina furaha usiku wa leo kwamba tunao Ujumbe huu. Nami nina furaha sana kwamba mlihudhuria, na kuhudhuria kwenu kumethaminiwa sana na mimi. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniruhusu nione yale ambayo nimeona, na kuweza kuuleta kwa kanisa hili, na sasa umetoka moyoni mwangu. Kwa muda fulani Roho Mtakatifu alishughulika na moyo wangu, nisingeweza kuuondolea mbali, ilinibidi tu niende Nao.

Kuna mambo mawili niliyojisikia kuongozwa kufanya.

280 Kwenda Shreveport, Louisiana, kwa ajili ya mkutano pamoja na Ndugu Moore. Naye mke wangu anayeketi pale anaweza kuwaambia. Kwa majuma kadhaa karibu nilie, "Ninataka kwenda Shreveport. *Kwa nini*?" Na mtu yeyote aliyekuwa huko Shreveport anajua ni *kwa nini* sasa. Kamwe hawakuwahi kuona wala kusikia kitu kama hicho. Wahubiri wakija kutoka kila mahali, Wabaptisti na wa aina mbalimbali. Mtu mmoja alisema ya kwamba alianza, akaweka mkono wake kwenye sanduku la barafu, ndipo Roho Mtakatifu akaja juu yake na kusema, "Nenda Shreveport, Louisiana, utaambiwa huko la kufanya." Akaambiwa jina langu na mahali pa kupata... Akasema, "Atakwambia la kufanya."

281 Nikasema, "Kidimbwi kimefunguliwa chini ya vile vipandio. Unahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu." Na pale...

282 Kwa hiyo mambo kama hayo, watu wakizungumza, na—na unabii na mambo ya kubashiri mambo yaliyotukia pale pale miongoni mwetu.

283 Ndipo nikasema, "Sina budi kwenda Jeffersonville na kukiandika kitabu hiki, maana sijui ni muda gani zaidi ninapaswa kuwa hapa. Bali nikiyaelezea Haya na yaandikwe, nikiisha kuondoka Maneno hayo yataendelea kuishi." Nimeiandika historia ambayo itaingia kwenye kitabu. Nami ninakuja hapa kuileta mbele ya kanisa kupata uvuvio wa Roho Mtakatifu, maana sikuyajua mambo haya mimi mwenyewe. Hiyo ni kweli. Hiyo ni katika Jina la Bwana, hiyo ni kweli, "sikuyajua."

284 Sasa najisikia kukombolewa, ninajisikia ya kwamba Mungu ametuletea Ujumbe. Ninaamini ya kwamba tuko mwishoni mwa safari, ninaamini ya kwamba wakati umewadia kwa ajili ya dhihirisho la Mungu kujulikana miongoni mwetu. Wala sijui itachukua muda gani zaidi, bali saa imekaribia.

285 Tutakuwa tukitarajia yule mtu mkuu kutokea. Anaweza akaja katika siku zangu, huenda akaja katika siku za walio vijana, sijui mimi. Huenda akawa papa hapa miongoni mwetu sasa, hatujui. Roho Mtakatifu yuko hapa kutuongoza hadi wakati huo, ndipo wakati kiongozi huyu atakapotuchukua atakuwa angali ametiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu; huyo—huyo Eliya atakuwa, hakika, ambaye atakuja. Bali atakuwa ndiye kiongozi atakayeigeuza mioyo ya watoto, ama, mioyo ya watoto iurudie Ujumbe wa Baba, irudi kwenye Ujumbe wa Baba yetu wa Mbinguni kwenye ile Siku ya Pentekoste wakati alipommwaga Roho Wake.

286 Ambapo mstari huo mdogo, niliuleta karibu sana nilivyoweza kwa historia na Biblia, na kuonyesha ya kwamba kitu hicho kimekuja moja kwa moja kupitia kwenye nyakati za kanisa, na hivyo ndivyo ilivyo leo hii, nikaonyesha ya kwamba madhehebu ni laana mbele za Mungu. Natumaini hilo limetatuliwa barabara niani mwenu, kwa Biblia, kwa matendo ya mitume, kwa historia na kila kitu. Hilo . . .

287 Wala kamwe hakuna wakati mmoja ambapo Mungu alipata kuliundia Kanisa Lake dhehebu. Mama ya makanisa yaliyounda dhehebu ni ukasisi wa Katoliki ya Kirumi. Kanisa Katoliki ya Kirumi, ndilo mama wa madhehebu. Na mara uamsho unapotokea katika kundi lolote la Kiprotestanti, wanarudi moja kwa moja na kufanya jambo lile lile. Nayo Biblia ilisema, “Yeye alikuwa ni kahaba. Naye, alikuwa na binti ambao walikuwa ni makanisa yaliyotoka kwake.” Ilibidi wawe ni wanawake, kuwa makahaba. Huyo hapo. Kwa hiyo tunaketi . . .

288 Lakini Yeye pia alisema hivi, “Msiogope, enyi kundi dogo, Baba yenu ameona vema kuwapa Ufalme.” Kwa hiyo naomba sisi sote, kwenye siku hiyo, ninyi Wamethodisti, Wabaptisti, chochote mlicho, “Kila atakayeufungua mlango, nitaingia na kula pamoja naye.”

289 Na tuhesabiwe, ndugu zangu, dada zangu, na tuhesabiwe kuwa kundi hilo dogo kwenye siku hiyo. Na tuwe sehemu ya kundi hilo dogo ambalo litakuwa likingojea hapo atakapokuja, atakapokuja kuwachukua kote ulimwenguni. Kwa—kwa kuwa Unyakuo utakuwa wa ulimwenguni kote. “Wawili watakuwa kitandani, nitamchukua mmoja; wawili watakuwa kondeni, nami nitamchukua mmoja.” Inaonyesha itakuwa usiku upande mmoja wa dunia na mchana upande huo mwingine, mnaona. Kwa hiyo, ni, “Wawili watakuwa kitandani, wawili watakuwa kondeni,” mnaona, “Nitamchukua mmoja-mmoja wa hao.”

290 Na kama nilivyosema asubuhi ya leo, utakuwa ukiendesha gari barabarani moja ya siku hizi, ukizungumza na mama, nawe utaangalia huku na huku, atakuwa ameondoka. Mtakuwa mmeketi mezani, mkinywa ka—kahawa yenu ama mkila kiamshakinywa chenu, ama—ama kitu fulani, na muda si muda

wajua, utaangalia huku na huku wala baba hayupo tena. Hiyo ni kweli kabisa. Unakuja, wala hatujui ni wakati gani. Bali jambo ni kwamba, utakapokwisha basi umekwisha, basi hakuna kitu kingine unachoweza kufanya kulihusu. Unasema, "Nimesikia hilo kwa muda mrefu." Lakini utalisikia kwa mara yako ya mwisho. Hiyo ni kweli. Litatukia kwa sababu ni Neno la Bwana. Pia, kumbukeni, je, limeshindwa wakati wowote katika siku hizi nane usiku ambazo nimekuwa nikihubiri? Lakini kile—kile Yesu alichosema hapa, kimetimia, na kila wakati wa kanisa umefanya vivyo hivyo hasa.

291 Nasi tunauona wakati huu wa kanisa umeingia moja kwa moja ndani yake, na kwenye saa ile ile. Hata asubuhi ya leo, katika kule kuwafananisha wale wanawali, wakati ule ule ambapo mwanamwali aliyelala. . . Sasa, kumbukeni, Biblia ilisema ya kwamba mwanamwali aliyelala. . . wakati kilio kilipotolewa, "Tazama, Bwana-arusi yuaja," kule kuja kwa Bwana, kuhubiriwa kwa Neno. Basi ilikuwaje? "Wakati umekaribia, mabomu ya atomiki, na kila kitu tayari," wahubiri wakikimbia mitaani na kuanza kuutangaza Ujumbe kwa sauti kuu.

292 Na mara wanapofanya hivyo, lile kanisa kubwa basi, mwanamwali aliyelala, alisema, "Aa, vema, tumekuwa Wapresbiteri kwa muda mrefu, labda tutasoma tupate kujua. Naam, mnajua, ninaamini kweli tunamhitaji Roho Mtakatifu." Nao wanaandika vijitabu na kila kitu kuhusu jambo Hilo sasa, wakianza. Nao walisema, "Mwaweza kutupa kidogo?"

Nao wakasema, "La, tuna ya kututosha tu sisi wenyewe."

293 Kwa hiyo walipoenda kutafuta Roho Mtakatifu, walipoenda kuomba kwa bidii, kama vile makanisa, yale makanisa makubwa mazuri yanavyofanya siku hizi, yale madhehebu. Walipoenda kununua Mafuta, Bwana-arusi akaja. Kwa hiyo wanajaribu kuyapata sasa hivi, makanisa makuu, madhehebu, mikutano mikuu ya kimataifa kuhusu jambo Hilo katika—katika makanisa ya kimadhehebu, wakisema, "Inatubidi kurudi kwenye zile Baraka za Kipentekoste. Hatuna budi kuwa na waponyaji wa kiungu kanisani. Hatuna budi kuwa na wanenaji kwa lugha. Hatuna budi kuwa na wafasiri wa lugha. Hatuna budi kuwa na karama zote hizi za kiroho kanisani mwetu, nasi inatubidi tu kuanza mikutano na kuanza kufanya jambo hilo." Wanafanya mabaraza, wameanza kufanya hivyo. Walipokuwa wameenda kufanya hivyo, ni kwenye wakati uo huo ambapo Bwana-arusi alikuja na kuwapata wale waliokuwa na Mafuta kwenye taa zao, nao wakaondoka.

294 Ndipo wakaja, na jambo gani lililotukia? Walitupwa kwenye giza la nje (ule wakati wa Dhiki Kuu) ambako kutakuwa na kilio na kuomboleza na kusaga meno, wakati Bibi-arusi akiwa Mbinguni. Loo, jamani!

295 Ndipo mwishoni mwa miaka hiyo mitatu na nusu, Yeye atakuja kama Yusufu alivyofanya na kujitambulisha kwa ndugu Zake. Itasababisha kilio kila mahali, nao watasema . . . Watazitenga familia zao, na kulia na—na kusema, "Ulipata wapi makovu hayo?" Na—na aliyechomwa . . . wale waliomchoma watamwona, Naye atajitambulisha kwa ndugu Zake.

296 Sasa Yeye anajaribu kujitambulisha kwa Kanisa Lake, nao wamemsukuma nje. Naye angali amesimama, akibisha, akisema, "Je, kuna mwingine mle ndani? Mtu ambaye angefungua na kuniruhusu niingie na kuzungumza nawe?"

297 Loo, nina furaha, ninashukuru sana kwamba yapata . . . miaka mingi iliyopita, yapata miaka ishirini na minane iliyopita, nilisikia huko kubisha moyoni mwangu. Nami . . . Yeye aliingia, nimekuwa nikila pamoja na Yeye na Yeye pamoja nami tangu wakati huo. Nami nilipokea Baraka za Kipentekoste, nikampokea Roho Mtakatifu.

298 Nilipobatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zangu, wakati pekee niliopata kubatizwa maishani mwangu, mara moja. Nilipokuwa mvulana mdogo tu, hakuna mtu angeweza kuniambia kulikuwako na Miungu watatu. La, usingeweza kushindilia hilo shingoni mwangu. Huwezi kumpa mtu yeyote anayejua lolote . . . anayejua kwamba Mungu ni nani. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo nilipobatiza . . . Mhubiri wa Kibaptisti aliponibatiza. Nilisema, "Ninataka kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo." Dk. Roy E. Davis alinibatiza katika Jina la Bwana Yesu Kristo wakati nilipokuwa mvulana tu. Mnaona? Hiyo ni kweli. Kwa hiyo ni—niliuamini, nimekaa nao, nami najua ni wa Kweli. Ni Neno la Milele la Mungu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema
mimi ni mmoja wao;
Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Ingawa huenda watu hawa wasielimike
wakawa,
Wala kujivunia umaarufu wa ulimwenguni,
Wote wamepokea Pentekoste yao,
Wakabatizwa katika Jina la Yesu;
Na wanatangaza sasa, karibu na mbali pia,
Nguvu Zake zingali ni zile zile,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao . . .

299 Je, una furaha? Kama unayo, inua mkono wako.

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;

(Mara unapokuwa Wake utakuwa juu ya dhambi zote, katika Jina la Yesu Kristo.)

Njoo, ndugu yangu, tafuta baraka hii
Itakayousafisha moyo wako kutokana na dhambi,
Itakayofanya kengele za shangwe zianze kulia
Na itaendelea kuiwasha moto nafsi yako;
Loo, inawaka sasa ndani ya moyo wangu,
Loo, utukufu kwa jina Lake,
Nami nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

Loo, mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao, Haleluya;
Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha juu,
Wote wakiomba katika jina Lake,
Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu,
Na nguvu za utumishi zikaja;
Sasa yale aliyowafanyia siku hiyo
Atakufanyia yayo hayo,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema . . .

300 Sasa hebu tupeane mikono, mbele, nyuma, na pande zote.

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

Loo, mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao;
Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao;

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema
mimi ni mmoja wao.

Hivi huna furaha ya kwamba wewe ni mmoja wao? [Kusanyiko linajibu, "Naam! Amina! Haleluya!"—Mh.] Napenda hilo. Kundi lenye kelele.

301 Shh! Shh! [Ndugu mmoja ananena kwa lugha nyingine. Ndugu mwingine anatoa ufasiri—Mh.] Jinsi tunavyokushukuru, Baba, kwa ajili ya wema na rehema Zako kwetu, tusiostahili. Kuwazia ya kwamba ungethibitisha Ujumbe Wako sasa, Bwana, uliowaahidi watu. Ninaomba, Mungu, ya kwamba rehema Zako ziwe juu yao.

302 Kukiwako na yeyote hapa asiyemjua kama Mwokozi, ungetaka kumpata sasa hivi moyoni mwako kama Mwokozi, waweza kusimama kwa miguu yako tunapokuombea? Yeye alisema ya kwamba angeninii. . .aliufanya Ujumbe huu hapo na alitaka kukuthibitishia Neno Lake. Kukiweko na wengine hapa wasiomjua wala hawajampokea Roho Wake, Yeye ananena nawe.

303 Vema, yule pale nyuma. Ungeweza kusimama kwa miguu yako, ndugu? [Ndugu fulani katika kusanyiko anazungumza—Mh.] Yeye anataka kubatizwa katika Roho Mtakatifu, sivyo, ndugu? Mungu akubariki. Simama mahali ulipo. Kuna mwingine ambaye angetaka kusimama na kusema, "Ningetaka kubatizwa katika Roho Mtakatifu"? Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Hilo ni jema. Simama tu kwa miguu yako. Endeleeni tu kusimama kwa miguu yenu. Huenda kuna mwingine ambaye angetaka kumpokea Roho Mtakatifu na kubatizwa, angetaka kukumbukwa katika maombi yetu sasa hivi, kubatizwa katika Roho Mtakatifu? Kuna mwingine, kabla sijasema kile ninachotaka kusema, angetaka kusimama na kujumuishwa pamoja nao?

Loo, ungetaka kuhesabiwa kama mmoja wa
kundi Lake? (Ungefanya hivyo?)
Uwe bila waa ndani, uwe ukikesha na kungoja
kuona lile tamasha;
Yeye yuaja tena.

304 Yuaja tena. Je, ungetaka kuwa adui Wake ama ungetaka kuwa mtoto Wake? Mungu mwenye hasira asubuhi hiyo, Yeye hatatambua kitu chochote ila Damu ya Yesu. Yeye kamwe. . . Ufuasi wako wa kanisa hautakuwa kitu Kwake. Hakuna kitu ila Damu!

Loo, mtiririko huo ni wa thamani
Unaonifanya mweupe kama theluji;

Polepole.

Sijui chemchemi nyingine,
Ila damu yake Yesu.

Ni nini iwezayo kuosha dhambi zangu?
Hakuna chochote ila damu yake Yesu;
Nini kinachoweza kunifanya mzima tena?
Hakuna chochote ila damu yake Yesu.

Loo, huo mtiririko ni wa thamani jinsi gani
Unaonifanya mweupe kama theluji;
Sijui chemchemi nyingine,
Hakuna chochote ila damu yake Yesu.

[Ndugu Branham anaanza kuuvumisha huo wimbo—Mh.]
Hakuna chochote ila damu yake Yesu;
Hii ndiyo haki yangu yote,
Hakuna chochote ila damu yake Yesu.

Kunaye mwingine?

Loo, wa thamani ni. . .(Hakuna kinachoweza kusimama, ndugu, dada. Ulimwengu unazama, umekwisha!)
. . .kama theluji;
Sijui chemchemi nyingine,
Hakuna chochote ila damu yake Yesu.

305 Pole pole, Teddy, ukiweza, "Kuna Chemchemi Iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli."

306 Sasa, enyi marafiki, ninyi mnaosimama kwa miguu yenu m—mnaojaribu kukubali utamu wa Bwana Yesu. Biblia iyo hiyo inayotwambia kwamba mambo haya yangetukia, iliyatimiza vile vile hasa alivyoahidi. "Sasa, ahadi" alisema Petro "ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

307 Ulisimama kwa sababu unataka baraka za Mungu juu yako. Na kama mtumishi Wake, ninakuombea, nitaomba ya kwamba Mungu atakupa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na sijui kama ungeweza kufanya hivi moyoni mwako, kama u mwaminifu, kama ungemtolea Mungu ahadi hii: "Mungu, mimi, tangu wakati huu, nikisimama kwa miguu yangu, nikiutafuta ubatizo huu wa Roho Mtakatifu, nitaendelea kuomba na kungoja hata utakaponijaza kwa Roho Mtakatifu." Mwaweza kumtolea Mungu ahadi hiyo kwa kuinua mikono yenu? "Sikuzote nitaomba, sikuzote, mpaka unijaze kwa utamu na wema wa Roho."

Ninakuombea sasa wakati tukiinamisha vichwa vyetu:

308 Baba yetu wa Mbinguni, hao ni kumbukumbu za Uwepo Wako. Wanajua ya kwamba Maneno haya ni kweli kwa sababu ni Yako. Wanajua ya kwamba yametolewa na Roho Mtakatifu, kwa sababu ni Neno la Mungu. Nao wameshawishika ya kwamba

wanakuhitaji Wewe, ya kwamba wanahitaji utamu wa Roho Mtakatifu maishani mwao kuwapa nguvu za ushindi. "Nao watapokea nguvu zitokazo Juu," watapokea nguvu za kuishi maisha ya Kikristo, kupokea nguvu za kushinda majaribu. Kama ule wimbo tuliokuwa tu tukiimba, "Walikusanyika katika chumba cha juu na walikuwa wakiomba katika Jina Lake, wakabatizwa kwa Roho Mtakatifu na nguvu za huduma zikaja." Hizo ndizo wanazotaka, nguvu za huduma zije juu yao.

309 Ninakuomba Wewe, Baba, kama mtumishi Wako, jinsi ulivyowaona wakiinua mikono yao, wamekutolea nadhiri na kuahidi ya kwamba hawatakoma kamwe, hawataweka kando, bali wataomba mpaka uwajaze, Bwana, kufikia kiwango cha kuridhisha cha Uwepo Wako Mtakatifu maishani mwao. Ninayatoa maombi yangu kwa niaba yao, Bwana, kama mtumishi Wako, kwamba watajazwa na Roho Mtakatifu. Bwana, ninaomba ya kwamba hawataondoka kwenye kanisa hili mpaka hilo litakapotendeka, kwamba watakuwa papa hapa mpaka kila nafsi imejazwa kwa Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana.

310 Wewe ni Mungu, Mwenyezi, ulidhihirishwa katika mwili kuziondoa dhambi za ulimwengu. Ulifufuka siku ya tatu, ukapaa Juu. Nawe uko hapa usiku wa leo, miongoni mwetu, na katika jina la Roho Mtakatifu. Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba Wewe, Bwana wetu wa thamani, utamjaza kila mmoja wao na Utu Wako Mwenyewe. Na jalia wao wawe ba—baraka kwa Ufalme Wako na katika ulimwengu ujao. Na siku moja hatimaye utakapofika mwishoni mwa safari, hiyo huenda ikawa ni leo hii bado, hatujui itakuwa wakati gani. Bali nijalie, Bwana; niweze kuhesabiwa miongoni mwa hao wanaoenda katika Unyakuo. Jalia hawa wawe ndio watakaoenda katika Unyakuo. Jalia kila mtu, Uwepo wa Kiungu na wote waliojazwa na Roho, ambao ni wa Mungu, waende katika Unyakuo.

311 Waingize hawa ndani usiku wa leo, Baba. Hao ni Wako sasa, ninawakabidhi Kwako. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

312 Sasa nawatakeni ninyi wengine mnaosimama karibu na watu hawa, mlio na Roho Mtakatifu, msimame, muwawekee mikono.

> . . . chemchemi iliyojaa damu,
> Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
> Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
>   mafuriko hayo,
> Hupoteza waa lao lote la dhambi.
> Hupoteza waa lao lote la dhambi,
> Hupoteza waa lao lote la dhambi;
> Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
>   mafuriko hayo,
> Hupoteza waa lao lote la dhambi.

Mwivi anayekufa alifurahia kuona
Chemichemi hiyo katika siku yake;
Na hapo naomba mimi, ingawa ni mwovu kama yeye,
Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu zote.
Nioshwe na kuondolea mbali dhambi zangu zote,
Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu zote;
Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya mafuriko hayo,
Hupoteza dhambi zangu zote.

313 Sasa mwinulieni Mungu mikono na mumpe tu sifa. Useme, "Asante, Bwana. Ninasimama kwa miguu yangu, nitakupa sifa. Nitakushukuru kwa ajili ya baraka Zako, kwa ajili ya wema Wako, na kwa kunipa ubatizo wa Roho Mtakatifu." Asante, Bwana! Asante, Bwana! Nakushukuru Wewe, Mungu mpendwa, kwa kutupa . . . Wewe hutimiza ahadi Zako, ulisema hivyo. Tunakuamini Wewe.

314 Hivi hamna furaha? Semeni, "Bwana asifiwe!" Teddy, hebu ninii . . . mwingine mmoja tu, "Tunakuta watu wengi wasioweza kuelewa . . . " *Hii Ni Kama Mbinguni Kwangu.*

Tunakuta watu wengi wasioweza kuelewa
Ni kwa nini sisi tuna furaha sana na ni huru;
Tumevuka Yordani tukaingia nchi nzuri ya Kanaani,
Na hii ni kama Mbinguni kwangu.

Loo, hii ni kama Mbinguni kwangu,
Loo, hii ni kama Mbinguni kwangu;
Loo, tumevuka Yordani tukaingia nchi nzuri ya Kanaani,
Na hii ni kama Mbinguni kwangu.

Loo, ninapofurahi, huimba na kupiga makelele,
Ibilisi haliamini hilo, naona;
Bali nimejazwa na Roho, hapana shaka,
Na hiyo ndiyo shida yangu.

Loo, hiyo ndiyo . . . Mbinguni kwangu, (Mungu asifiwe!)
Loo, hii ni kama Mbinguni kwangu;
Nimevuka Yordani nikaingia nchi nzuri ya Kanaani,
Na hii ni kama Mbinguni kwangu.

315 Si linawafanya kufurahi? Vema. Peana mikono na mtu fulani, useme, "Bwana asifiwe!" Hii ni kama Mbinguni, Bwana.

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na majonzi;
Litakupa furaha na faraja,
Peleka kila uendako.

Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Katika Jina la Yesu nainamia,
Nikisujudu miguuni Pake,
Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa Wafalme,
Safari yetu itakapokamilika.

Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo, ni tamu jinsi gani! (Ni tamu jinsi gani!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Sasa, kwa utulivu, huku vichwa vyetu vimeinamishwa:

. . .jina la Yesu daima,
Kama ngao dhidi ya kila mtego;
Majaribu yakikuzunguka,
Litamke tu Jina hilo takatifu katika maombi.

Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!

Wakati wa Kanisa La Laodikia SWA60-1211E
(The Laodicean Church Age)
Mfululizo wa Ufunuo Wa Yesu Kristo

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili jioni, Desemba 11, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org